# ULIMWENGU UNAPOROMOKA TENA

Amina. Bwana awabariki. Mnaweza kuketi. Ilisikika ya kupendeza sana kuingia hapa usiku wa leo na kuwasikia mkimsifu Bwana, na kurudi nyumbani tena na kumwona kila mtu. Nimekuwa nikitazamia hili tangu Shukrani iliyopita nilipokuwa hapa, kurudi kwenye maskani yangu tena. [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Sijui mahali alikoenda. Hapa huyu hapa. Nashangaa tu ikiwa alikuwa bado anaenda kusema "amina" kwa hilo, mwajua. [Ndugu Moore anasema, "Amina."] Daima ni vyema kuwa hapa. Nami nilitazamia, kama nilivyosema, tangu Shukrani iliyopita.

2 Ndiyo kwanza tutoke kwenye Mji wa New York, ambapo tulikuwa na kampeni ya ajabu. Bwana alitubariki huko kwa njia kuu. Na tulikuwa kwenye Ukumbi wa Morris, na umati ukajaa, na huku na huko mitaani. Na wangesimama huko nje, wakingojea. Kama—kama mmoja angeingia, mtu tu anayesimama karibu, mwajua, na angewazia, vema, jambo fulani; watu wengine, mnajua, huenda kanisani, halafu jambo la kwanza, jambo fulani likisemwa, ambalo hawalipendi, watasimama na kuondoka. Basi walikuwa huko nje wakipiga kura, ni nani angekipata kiti hicho wakitoka nje. Nami nikaja pale kila usiku, na karibu umbali wa jengo la mji, nao wangelundikana huku na huko mitaani. Naye Bwana alitubariki na kutupatia nafsi, na uponyaji mwingi mashuhuri ulitendeka.

3 Halafu basi kwenye kiamshakinywa cha Wafanyabiashara, tulikuwa na wakati mzuri, wakauza tikiti zao. Ndipo—ndipo basi nafikiri iliwabidi kuingiza ndani mamia, ambao hawakuwa na tikiti. Kisha wakajaza vichochoro, na kuzunguka ukumbi na milango, na kadhalika. Na sisi tulikuwa tu na wakati mzuri. Kasisi wa Kiepiskopolia na kila kitu pale, naye Bwana akatubariki kwa njia kuu.

4 Ndipo basi tulisimama kwenye nyumba, nyumba yangu nyingine, huko Jeffersonville. Bila shaka, ninaishi sasa Tucson, Arizona, kama mjuavyo, kwa miaka miwili iliyopita.

5 Na sasa niko njiani kurudi Tucson sasa, kwa ajili ya kiamshakinywa cha Wafanyabiashara juma lijalo huko Phoenix. Ambapo, moja kwa moja baada ya siku ya kwanza ya mwaka, tunaanza kampeni kule, siku chache kabla ya mkutano wa Kimataifa wa Wafanyabiashara, ninaamini, ama mkutano wa kitaifa kwenye—kwenye Hoteli ya Ramada.

6 Na ni vyema sana kuwa hapa katika—katika mji huu mzuri wa Shreveport, usiku wa leo.

7 Sasa, kwa kawaida mimi huzungumza kwa muda mrefu. Bali ninaenda kujaribu niwezavyo kuufupisha, saa tatu au nne, hata hivyo, kwa huu na kwa wakati huu. Basi ninajua tu kwamba mimi huwachosha kabisa, bali, mnaona, sipati kuwaona mara kwa mara. Na wengi huenda Nyumbani kabla mimi... wanaenda Nyumbani Utukufuni kabla sijaweza kuwaona tena, na mimi ninawazia, "Vema, haya yatakuwa ndiyo maongezi yetu ya mwisho duniani kabla hujaruka na kuenda." Na wengi wameenda, hapana shaka, tangu wakati huu mwaka uliopita. Na labda, Bwana akikawia, na tuweze kurudi tena mwaka ujao au wakati mwingine, itakuwa ni wengine zaidi, hapa usiku wa leo, labda mimi mwenyewe. Hatujui ni wakati gani tutakapoitwa. Pia, mnajua, Bwana Yesu huenda akaja hata kabla ibada hizi kufungwa usiku wa leo.

8 Sasa, kama mnavyonijua, mimi si mzungumzaji hodari, mimi si mnenaji. Ni—ninampenda tu Bwana na kufanya kile niwezacho kwa ajili ya utukufu Wake. Basi ninaposimama hapa katika jukwaa hili, nikijua kwamba watu kama Ndugu Moore na watu wengi mashuhuri wamesimama kwenye jukwaa hili, hunifanya nijihisi kwa namna fulani—kwa namna fulani...si kuwa mahali pasipostahili, simaanishi hilo. Ila, ninamaanisha, sarufi yangu na kadhalika, ninajihisi, kama watu hawakunipenda vizuri sana, wangesimama na kuondoka nilipoingia mimbarani. Kwa hiyo wanavumiliana tu nami, nami ninashukuru kwa hilo. Sasa...

9 Lakini kila mara mimi huja na le—lengo hili. Siji hapa ili tu kuonekana; kama ningekuja hivyo, ningeenda nyumbani kwako kwa matembezi, unaona. Ninakuja hapa kufanya vizuri sana niwezavyo kwa ajili ya Bwana Yesu Kristo, wakati nikiwa hapa. Nipo hapa si kwa kusudi lolote jingine ila kumtumikia Yeye, na vizuri zaidi nijuavyo, na kuwaleteeni Neno jinsi tu nilivyopewa, kuwaombea wagonjwa wenu na wanaoteseka. Sasa, tutakuwa na siku moja, au mbili usiku, mimi na Ndugu Moore tutakuja pamoja, kwamba tunaenda kuwaombea wagonjwa.

10 Basi, kila usiku, tunataka kila mtu ambaye si Mkristo, natumaini jambo fulani litasemwa au kufanywa, hata utakuwa Mkristo. Na kama wewe siye, ikiwa tayari umemwamini Bwana Yesu Kristo, na kumkubali na umebatizwa, wala hujapokea Roho Mtakatifu bado, usiache hili lipite. Acha tu huu uwe usiku wako. Kwa sababu, kumbuka, kutakuwa tu na majina kiasi kwenye Kitabu hicho. Na wakati jina la mwisho likiongezwa, huo ndio mwisho. Na lako huenda likakamilisha Hicho.

11 Wakati Mwana-kondoo alipokuja na kukitwaa Kitabu kutoka kwa mkono wa kuume wake Yeye aliyeketi juu ya Kiti cha enzi, hicho kilikuwa ni Kitabu cha Ukombozi. Na majina

hayo yaliwekwa humo ndani kabla ya msingi wa ulimwengu. Wakati hilo jina la mwisho lilipoitwa, Kitabu, mpango, kila kitu kingine kilifunuliwa wakati huo, Mihuri Saba ilifunuliwa na Mwana-kondoo. Siri za Biblia nzima zilifichwa Humo ndani. Kama tungalikuwa na wakati, ningependa kuninii . . .

12 Ndiyo kwanza tumalize hiyo Mihuri Saba, hivi majuzi tu. Ningependa kuipitia tena. Na jinsi tu ambavyo Bwana alitubariki! Wengi wenu mmesikia kuhusu hiyo, na kusoma katika jarida la *Life*, na kadhalika, mambo yaliyotokea wakati huo. Wakati, walipoipiga picha, hata, ya hao Malaika saba, ilivyobashiriwa tulipoelekea Magharibi. Na Yeye aliniambia, miezi mitatu hapo kabla, mahali ingekuwa na jinsi ambavyo ningekuwa nimesimama hapo, nayo hiyo hapo! Nazo ka—nazo kamera, loo, kwa mamia ya maili, walipiga picha Yake pale pale, hasa kabisa. Ilibashiriwa hakika! Na kama niliwahi kuhubiri chochote kilichovuviwa, maishani mwangu, ni *Ile Mihuri Saba*. Na kwa hiyo ninajua tuko kwenye wakati wa mwisho.

13 Basi jina la mwisho linaingia kwenye Kitabu hicho, ama, jina la mwisho linalokombolewa, lililowekwa kwenye Kitabu hicho, hilo latosha, Yeye anakuja kudai kile alichokomboa. Na huenda ukawa ni wakati wa kigeni. Hivi uliwahi kuwazia: watu wataendelea moja kwa moja kuhubiri, kanisa litaendelea moja kwa moja hata kufikiria kwamba wanafanya watu kuokoka. Imechelewa kupita kiasi wakati huo, yote yamekwisha, unaona, ndipo Ujumbe utawaendea waliopotea kabisa; kama tu ulivyofanya katika siku za Nuhu, siku saba ndani ya safina. Ulifanya katika siku za Sodoma. Yesu Mwenyewe, hatua Ya—Yake ya tatu ya huduma Yake, Yeye alienda na kuzihubiria nafsi zilizokuwa zimepotea Milele, zilizokuwa kifungoni, ambazo hazikutubu, uvumilivu katika siku za Nuhu. Nasi hatujui ni wakati gani mambo haya huenda yakatokea.

14 Na hebu tuonywe. Usisimame tu karibu, hebu tufanye jambo kulihusu. Kama hatuko sawa na Mungu, hebu tuwe sawa na Mungu.

15 Wakati mmoja, nafikiri, katika mlango wa 11 wa Mathayo, ninaamini ndivyo, yapata kifungu cha 6, au kitu fulani, sina hakika na hilo. Ni mlango wa 11, nina hakika kabisa. Wanafunzi wa Yohana walitumwa na Yohana, wakati mmoja, kumwona Bwana Yesu, kumwuliza ikiwa Yeye kwa kweli alikuwa ndiye Yule, ama wamtazamie mwingine. Yeye akasema, "Nendeni mkamwonyeshe Yohana mambo yanayofanyika. Mwambieni, 'Amebarikiwa yeye asiyechukizwa na Mimi.'"

16 Ndipo basi wakati walipovuka kilima, na Yesu labda aliwaangalia, Yeye alisema, "Mliondoka kwenda kuona nini?" Na wao . . . Kasema, "Je! mlienda kuona namna fulani ya mtu aliyevikwa mavazi mororo?" Akasema, "Hao wako kwenye ikulu za wafalme. Na unyasi unaotikiswa na upepo?" Akasema, "Hivi

mlienda kumwona nabii?" Kasema, "Nawaambieni, na zaidi ya nabii. Kama mnaweza kulipokea, huyu ndiye ambaye nabii alinena habari zake, Malaki 3, 'Nami nitamtuma mjumbe Wangu mbele ya uso Wangu.'"

17 Wanafunzi waliuliza wakati mmoja kuhusu swali hili. Wakasema, "Ni kwa nini waandishi wanasema, walimu wa Maandiko, kwamba, 'Imempasa Eliya kuja kwanza kabla ya haya, mambo haya yote kutendeka'?" Sasa kumbukeni, Yeye alikuwa anazungumza na wanafunzi, si Mafarisayo. Wanafunzi, walisema, "Ni kwa nini waandishi wakasema hivyo, 'Imempasa Eliya kuja kwanza'?"

18 Akasema, "Eliya amekuja tayari, nao walimtendea yote waliyotaka, nanyi hamkujua."

19 Vipi kama siku moja ungegundua, tungeingia katika wakati wa dhiki ama kitu fulani, unasema, "Vema, nilidhani Unyakuo ulikuwa uje kwanza"? Unaona? Ndipo sauti itanena na kukuambia, "Unyakuo ushafanyika, nawe hukujua."

20 "Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, ambapo watu wanane waliokolewa kupitia maji, ndivyo itakavyokuwa katika Kuja kwa Mwana wa Adamu." Watu wanaendelea moja kwa moja, wakidhania tu kuwa wanafanya tu jambo linalofaa, na yote yatakuwa yamekwisha. Ee Mungu, turehemu! Hebu, hebu tujichunguze, hivi sasa katiku siku hizi chache usiku, tuone mahali tulipo.

Hebu tuinamishe vichwa vyetu tena.

21 Bwana Yesu, tukiwa na mambo haya niani, na kuwasilishwa kwa kanisa hili, kuwasilishwa kwa watu hawa; Mungu, ninaomba ya kwamba Wewe utaokoa kila nafsi iliyoko Shreveport, wakati huu, iliyoandikwa kwenye kile Kitabu. Iwapo kuna wengine hapa ambao hawajaokoka, Baba, jalia hii iwe ndiyo saa ambayo wanaokoka. Kama kuna yeyote katika kusanyiko hili, usiku wa leo, jalia huu uwe ndio usiku wao.

22 Mbariki Ndugu Moore, Dada Moore, na familia yao, watoto wao, watoto wa watoto wao. Mungu, tunakushukuru tu Wewe kwa ajili yao. Na Ndugu Lyle, Ndugu Brown na ndu—ndugu wote hapa kanisani, Ndugu Don, na kundi hili zuri la watu, washiriki wote hapa, walei, tunakushukuru tu Wewe kwa ajili yao.

23 Pia tunaomba, Baba wa Mbinguni, kwamba kukutanika kwetu pamoja hapa kwenye hii Shukrani. . .Huenda ikawa ndiyo Shukrani ya mwisho tutakayowahi kukutanika pamoja hapa duniani, kwa hiyo, Mungu, tujalie kutumia kwa manufaa na kutunza wakati. Tena tunatambua kwamba ku—kunachelewa, nasi tunataka kila kitu tuwezacho kufanya, kilicho katika uwezo wetu, ili kutimiza kazi kwa ajili ya Bwana Yesu kabla hajaja. Kwa njia fulani, kwa namna fulani ninahisi kwamba Yeye anatungojea sisi ku—kuimaliza kazi. Kwa hiyo, tusaidie, Bwana, usiku wa leo, kama mtu binafsi, kila mmoja

wetu, kwamba tuweze kuwajali sana wengine, hata tuende nje mitaani, ama katika ujirani, na—na kuwaingiza waliopotea, ili waweze kuokolewa.

24 Libariki Neno Lako. Neno Lako ni Kweli, Bwana, Kweli yote. Kwa hiyo tunaomba, kwamba tunapojaribu kufanya kila jitihada kumega Mkate huu wa Uzima, Kweli, kwa watu, kwamba Roho Mtakatifu atakuja, kwa sababu ya mwili huo uliovunjwa pale Kalvari ambapo ilibidi dhambi iuvunje, na atajigawa Mwenyewe miongoni mwetu tena, katika ushirika kwenye Neno. Kwa kuwa tunaomba hayo katika Jina la Yesu. Amina.

25 Sasa, mkipenda, ninataka mgeuke pamoja nami. Wengi wenu hupenda kwa namna fulani kuhifadhi Ma—Maandiko ambapo mhudumu anasoma, ama mwinjilisti. Nami ninataka kusoma baadhi, usiku wa leo, kutoka Kumbukumbu la Torati, mlango wa 4, kuanzia kifungu cha 7 hadi cha 14. Pia Kitabu cha Waebrania, mlango wa 14, kifungu cha 25 mpaka cha 29, pamoja. Kumbukumbu la Torati 4.

> *Kwa maana liko taifa gani kubwa, lililo na Mungu aliye karibu nao, kama BWANA Mungu wetu alivyo katika mambo yote tunayomwitia?*
>
> *Tena liko taifa gani kubwa, lililo na amri na hukumu zenye haki kama torati hii yote, ninayoiweka mbele yenu leo?*
>
> *Lakini jihadhari nafsi yako, ukailinde roho yako kwa bidii, usije ukayasahau mambo yale uliyoyaona kwa macho yako, yakaondoka moyoni mwako siku zote za maisha yako; bali uwajulishe watoto wako na watoto wa watoto wako;*
>
> Hasa *siku ile uliyosimama mbele za BWANA Mungu wako huko—huko Horebu, BWANA aliponiambia, Nikusanyieni watu hawa, nami nitawasikizisha maneno yangu, ili wajifunze kunicha mimi siku zote watakazoishi duniani, wakapate na kuwafundisha watoto wao.*
>
> *Mkakaribia, mkasimama chini ya ule mlima; mlima ukawaka moto mpaka kati ya mbinguni,* kwa *giza* na *mawingu, na* uzito, na *giza kuu.*
>
> *BWANA akasema nanyi kutoka kati ya moto; mkaisikia sauti* Yake *ya maneno, lakini hamkuona umbo lolote; sauti tu.*
>
> *Akawahubiri agano lake, alilowaamuru kulitenda, yaani, zile amri kumi; akaziandika juu ya mbao mbili za mawe.*

> *Bwana akaniamuru wakati ule niwafundishe maagizo na hukumu, mpate kuzitenda katika nchi* ile *mtakayoivukia ili kuimiliki.*

26 Na sasa katika Kitabu cha Waebrania, mlango wa 14, kuanzia kifungu cha 25.

> *Angalieni msimkatae yeye anenaye. Maana ikiwa hawakuokoka wale waliomkataa yeye aliyenena juu ya nchi, zaidi sana hatutaokoka sisi tukijiepusha na yeye* anenaye *kutoka mbinguni;*
>
> *Ambaye sauti yake ilitetemesha nchi wakati ule; lakini sasa ameahidi akisema, Mara moja tena* nitatetemesha, *nitatetemesha si nchi tu, bali na mbingu pia.*
>
> *Lakini neno lile, Mara moja tena*. . .ladhihirisha *kuhamishwa*. . .*vile viwezavyo kutetemeshwa, kama vitu vilivyoumbwa, vitu visivyoweza kutetemeshwa vikae*. Hapo. . .
>
> *Basi kwa kuwa* tunapokea *ufalme usioweza kutetemeshwa, na mwe na neema, ambayo kwa hiyo tumtolee Mungu ibada ya* kumpendeza, *pamoja na unyenyekevu na kicho;*
>
> *Maana Mungu wetu ni moto ulao.*

27 Sasa ninao muhtasari mdogo hapa, na Maandiko fulani niliyoandika, ambayo ningetaka kurejea kwa dakika chache, kama vile ningeupa huu maskini mada ya ajabu. Na kanda hizi ziko tayari wakati wowote mtu yeyote angezihitaji. Bw. Maguire hapa ataweza ku—kuwapeni vitu hivi. Nami ninataka kuchukua fungu, kutoka kwenye fungu la somo hili, hasa, namna hii, *Ulimwengu Unaporomoka Tena*.

28 Tulikuwa tunateremka jana, ama jana jioni, kupitia Memphis, Tennessee, tukaingia kule kidogo wakati wa alasiri ukiisha, ama sehemu ya jioni. Na ilikuwa vigumu kwetu kupitia mitaani, wa—watoto na watu walikuwa wamesongamana sana. Ndipo nikawaza, "Hii inaweza kuwa ni kitu gani?" Wa—watu hawakuwa wamevalia kama kwamba walikuwa wamehudhuria mkutano wa kidini kama vile labda ndugu yetu mwema, Billy Graham au Oral Roberts. Nami sikufikiria walikuwa katika wilaya hiyo wakati huo, hata hivyo. Nao wanawake walikuwa wamevaa suruali fupi, na watoto wadogo karibu nao, walikuwa tu wamevalia surupwenye, na kadhalika, makabuti. Basi nilishangaa ilikuwa ni nini, ndipo hatimaye tukagundua. Walikuwa wamekuwa na gwa—gwaride ya Baba Krismasi. Kulikuwa na maelfu mengi walikuwa wanaitazama mitaani, na kadhalika. Nasi tulikuwa tu na wakati mgumu sana kupitia Memphis, kwa sababu inakaribia wakati wa Krismasi.

29 Nayo Krismasi ni siku kubwa sana ya biashara, mpaka karibu imeondolea mbali kabisa Shukrani, kwa sababu... katika—katika ulimwengu wa biashara, hata hivyo; kwa sababu kwamba u—ulimwengu wa biashara umeshawishiwa sana na Krismasi, kwa sababu kuna watu wengi sana wanaonunua. Nao wananinii tu...Shukrani kidogo inapita. Na tunaona, tunapoona Krismasi ikikaribia tena, nilifikiri lingekuwa ni jambo jema kuzungumza juu ya somo hili, tunapoikaribia. Tukiona kwamba, kwa kweli, Krismasi si...

30 Tunasherehekea siku hii ya 25 ya Desemba kwa ajili ya siku ya kuzaliwa kwa Kristo, bali, kwa kweli, mtu yeyote anajua ya kwamba haikuwa siku ya kuzaliwa kwa Kristo. Hiyo ilikuwa ni siku ya kuzaliwa kwa mungu-jua wa Rumi, ambapo kanisa lilipobadilishwa kuingia, au, kuingizwa katika Ukatoliki, iliundwa kwenye baraza huko Nikea. Badala ya hiyo kuwa ya "mungu-jua," waliifanya siku ya kuzaliwa kwa "Mwana wa Mungu." Huo ulikuwa ni wakati, jua, ni kuanzia tarehe 20 mpaka...ninamaanisha tarehe 21 hadi 25, kwa namna fulani liko kwenye ninii yake...Nasahau ni jina gani mnaiita, hasa. Ni wakati labda ni mara mbili au mara ya pili linapopita katika hatua hiyo. Na ilikuwa ni siku ya kuzaliwa kwa mungu-jua, nao wakachukua tu "Mwana wa Mungu" na kufanya hiyo siku ya kuzaliwa Kwake, kuioanisha na desturi yao ya kikafiri. Na hakuna njia, hata kidogo, hiyo kuwa siku ya kuzaliwa kwa Kristo.

31 Asingeweza kuzaliwa wakati huo, kwa sababu Uyahudi uko karibu sawa kwenye—kwenye ninii...juu kwenye ikweta, kama hii ilivyo, na sisi—sisi tunaona kwamba, katika Uyahudi, wakati wa baridi kali, tarehe 25 Desemba, una dhoruba kali ya theluji na baridi. Wachungaji hawawezi kuwa juu ya kilima, na sababu nyingi isingeweza kuwa.

32 Halafu basi Yeye alizaliwa kimaumbile, kama vile maumbile mengine yote, Yeye—Yeye alikuja katika majira ya Kuchipua. Kwa kawaida wakati wana-kondoo wanapozaliwa, majira ya Kuchipua; na Yeye alikuwa ni Mwana-kondoo. Sasa, ninaamini, Yeye alizaliwa, mimi mwenyewe, Machi, Aprili, ama mahali fulani karibu hapo, mwanzoni mwa majira ya Kuchipua.

33 Lakini tunaona kwamba walifanya siku ya biashara kutokana nayo. Watu wakisongamana mitaani, na kukosana, na kuzozana juu ya vitu, na kushangaa kuhusu kumpa mtu fulani zawadi, ni kiasi gani watakacholipa kwa hiyo.

34 Hivi majuzi, nilishangazwa. Mahali nilipokuwa nimesimama, na mama wawili walikuwa wakizungumza kuhusu kumpa baba yao ninii ya siku ya kuzaliwa...ama zawadi ya Krismasi kwa ajili ya mwaka huu. Ndipo mmoja wao akasema, "Nimemnunulia kisaga cha wiski." Na huyo mwingine akasema, "Nimemnunulia pakiti, au katoni ya sigara," au kitu kingine

namna hiyo. Nao walikuwa wakisema, mmoja alitoa zaidi sana kwa wiski kuliko walivyofanya kwa sigara.

35 Nami nikawazia, "Kama hiyo si njia ya kutoa ninii—ninii. . .kubadilishana au kutoa zawadi katika ukumbusho wa Yesu Kristo, Mwana wa Mungu!" Jinsi kilivyo kitu cha kujitafutia mauti!

36 Na mimi ninaona ulimwengu wetu katika huzuni kama ulivyo sasa, umechafuliwa kutoka kila upande, hakuna njia ulimwenguni kwao kuwahi kamwe kujirudia tena. Heri tujihadhari, kile tunachofanya katika siku hizi. Kwa kuwa tunao, hivi sasa katika maombolezo, ya mmoja wa misiba mikubwa mno, na—na moja ya ninii kuu. . .Hatukufikiria kamwe kitu hicho kingeweza kutukia Marekani, lakini kipo hapa kwa vyovyote vile. Na ulegevu wetu wenyewe kwenye Injili, imeliwa na wadudu pamoja na mambo kama hayo, na itakuwa mbaya zaidi. Hapana shaka hata kidogo, niani mwangu, ila kwamba itaendelea kuwa mbaya zaidi.

37 Lakini tunaona, kwenye Krismasi hii, kufikia kwenye somo, kwamba Krismasi hii inaukuta ulimwengu karibu tu kama ilivyofanya miaka elfu mbili iliyopita, wakati Yesu alipokuja. Haujabadilika sana tangu wakati huo. Maana, hii, Krismasi ile iliukuta ulimwengu ukiporomoka, nao ulikuwa unatazamia Masihi kusaidia kuushikilia pamoja. Na—na hivyo karibu ndivyo ulivyo leo hii, tunafanya jambo lile lile. *Ulimwengu Unaporomoka Tena*.

38 Sasa, hiyo siyo tu Marekani hapa, lakini hiyo ni kote ulimwenguni, popote uendapo; ulimwengu wa kidini, ulimwengu wa kisiasa, kila kitu, u—ulimwengu wa maadili. Hiyo—hiyo, hakuna tu zaidi ya hiyo, ni ninii tu. . .Maadili yako tu miongoni mwa watu wema, tena, na hayo ni vigumu sana kupata. Ni—ni aibu. Na siasa na kila kitu vimechafuka, mpaka kitu hicho chote ni kigonjwa na vidonda vyenye usaha, tangu kichwani hadi miguuni, ulimwengu wote. Mfumo wetu wa kisiasa, mfumo wetu wa kidini, mfumo wetu wa kiadilifu, kila kitu tulicho nacho, kimekwisha! Ninii tu, hakuna njia yoyote ya kuushikilia pamoja. Huo, huo umekwisha! Ninii. . . Tuko kwenye mwisho wa barabara. Ni hayo tu kwa hilo.

39 Sisi, ninajua tulizungumza juu yake muda mrefu, bali moja ya siku hizi litakuwa limepita kuzungumzia, litakuwa ni jambo la wakati uliopita, nasi tutajikuta wenyewe nje tusipoangalia wakati huu.

40 Sijui, kama sisi Krismasi hii, ikiwa Mungu angemtuma tena kama alivyofanya kule nyuma miaka elfu mbili iliyopita, kama Yeye angemtuma kwetu katika 1964, sijui kama tusingemtendea kama walivyofanya wakati ule? Nashangaa tu ikiwa Kuja Kwake kungekuwa zaidi, kama Yeye angekaribishwa zaidi, katika—katika—katika ulimwengu wa kisiasa au katika ulimwengu wa

kidini, zaidi ya alivyokuwa wakati ule? Sijui tu kama tuko zaidi katika hali ya kumpokea Yeye, kama alivyokuwa wakati ule? Lakini tunajua Yeye alikataliwa wakati ule.

41 Tungeweza kumfanyia nini kama angekuja? Labda ulimwengu wa kidini, ambao ninawekea msingi jambo hili, ungemfanyia kama ulivyofanya wakati ule mwingine. Wangemsulubisha kama wangeweza, (hawajabadilika), kwa sababu ile ile waliyofanya wakati ule mwingine.

42 Ni kwa nini walifanya hivyo, hivi walimsulubisha Yule hasa waliyekuwa wakiomba aje duniani, kuwaokoa, kuwaondoa kwenye mchafuko? Walisulubisha tumaini pekee walilokuwa nalo. Kwa nini? Ni kwa nini walifanya hivyo? Kwa sababu, wakati Mungu alipoyajibu maombi yao, Yeye aliyajibu katika njia ambayo hawakuyatarajia kujibiwa. Wakati Yeye alipokuja, Yeye hakuja katika ladha ya theolojia yao.

43 Basi kama Yeye akija tena, leo, Yeye angekuja kwa njia ile ile; nje ya ladha ya ulimwengu au theolojia ya makanisa, na jinsi ambavyo wangewazia kumhusu. Yeye daima huja. Kama watu wa Mungu, wakiingia taabuni, na kuomba, basi Mungu huwapa kile wanachoombea, ila Yeye hukitoa kwa njia iliyo nzuri kwao. Nao walikataa Hicho, kwa sababu Hicho hakiji katika njia ile wanayofikiria Hicho kinafaa kuja. Walilikataa Neno la Mungu lililopakwa mafuta, na Yeye ni Neno.

44 Sasa, Mungu, katika vizazi vyote, katika nyakati zote, wakati Yeye alipoanza, "Wakati Yeye aliponena Neno Lake katika nyakati mbalimbali kupitia manabii, katika siku hizi za mwisho kupitia Yesu Kristo, Mwana Wake," tunaona ya kwamba kila mmoja wa nabii hizo ulikuwa ufae wakati fulani. Kama vile Mfalme Nebkadreza wakati alipokuwa na hii ndoto, na ulimwengu wa Mataifa kuanzia kichwani hadi miguuni, naye Danieli akatoa tafsiri ya ndoto hii; huo ulikuwa u—unabii kwa ulimwengu wote, daima, kila sehemu ya Ufalme wa Mataifa, jinsi ambavyo ingekuja kuanzia kichwani hadi miguuni. Nao manabii daima wamenena Maneno yanayopaswa kutendeka katika kila wakati. Ndipo wakati Mungu . . .

45 Watu huingia katika shida, na Mungu huwajibu. Yeye huwatumia nabii aliyepakwa mafuta ama namna fulani ya mjumbe, kwa sababu Yeye hawezi kughairi Neno Lake ambalo Yeye amekusudia kwa wakati huo. Bali, kile ambacho Yeye hufanya, Yeye humtuma mjumbe kuifanya sehemu hiyo ya Neno kuishi kwa ajili ya wakati huo. Daima anafanya hivyo, unaona. Yeye alilifanya Neno Lake hapo mwanzo. Alijua mwisho tangu mwanzo. Alilinena Neno Lake. Na kila wakati, wakati wakiingia katika shida, wangeninii . . . wangeomba, naye Mungu angemtuma mmoja aliyepakwa mafuta. Na huyo aliyepakwa mafuta angeifanya kabisa ahadi hiyo kwa ajili ya wakati huo, ambayo ilitabiriwa kwa ajili ya wakati huo, iishi. Na hicho

ndicho Yeye hufanya wakati wote. Mungu daima habadilishi mpango Wake. Sasa, kamwe hatumwoni Mungu akibadilika.

46 Mungu aliimaliza wakati mmoja, jinsi Yeye angemwokoa mwanadamu, hiyo ilikuwa ni katika bustani ya Edeni, chini ya damu iliyomwagika. Tulijaribu kila mfumo mwingine, kuanzia majani ya mtini hadi elimu, saikolojia, madhehebu ya mifumo, na kadhalika, na kila moja ya hivyo ime—imekataliwa; wala haijafanikiwa, kamwe haitafanikiwa. Mungu atakutana tu na mwanadamu chini ya Damu iliyomwagika, na hapo ndipo mahali pekee ambapo atawahi kukutana na yeye, kwa sababu huo ulikuwa ndio uamuzi Wake wa kwanza. Kamwe hatakutana na mwanadamu chini ya mfumo wowote wa kimaadili. Hatawahi kamwe, hakuna njia ulimwenguni! Rudi tu moja kwa moja kwenye Njia ya Mungu, hiyo ndiyo Yeye alisema mwanzo. Na Yeye hana mwisho, hawezi kubadilika, na Yeye daima ni yeye yule. Hapo ndipo Yeye hukutana na mwanadamu, na hapo pekee. Hiyo ndiyo sababu tunashindwa kuwa na ushirika leo hii, hiyo ndiyo sababu kanisa limegawanyika sana, kwa sababu kila mmoja amejitenga katika mfumo, na, wanapofanya hivyo, basi Mungu huwakataa, papo hapo. Yeye anatutaka tukutanike chini ya Damu, mahali tuna vitu vyote shirika, chini karibu na Msalaba. Kusudi la pekee la Mungu la kufanya hivyo! Mungu daima hutuma Neno Lake.

47 Pia tunaona, leo, kwamba ulimwengu leo ni kama tu ulivyokuwa katika siku ile; ukijikuta wenyewe, mfumo wake wa kisiasa, na kadhalika, wote unaporomoka, na kumtazamia masihi ambaye ataushikilia pamoja.

48 Sasa, neno *masihi* maana yake "aliyepakwa mafuta," kitu kilichopakwa mafuta. Mungu! *Huu* ndio ufunuo wa Yesu Kristo, kitabu chote kilifungwa kwa Mihuri Saba ya ufunuo wa Yesu Kristo. Yesu Kristo alikuwa katika Mwanzo; Yesu Kristo alikuwa katikati ya Kitabu. Yesu Kristo alikuwa katika—katika Kutoka na Mwanzo, na Yeye alikuwa katikati ya Kitabu na Yeye alikuwa katika—katika Agano Jipya, na katika Ufunuo na moja kwa moja mpaka mwisho, "yeye yule jana, leo, na hata milele." Yote ni Mungu!

49 "Hapo mwanzo alikuwako Neno, naye Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno alifanyika mwili akakaa katikati yetu."

50 "Mungu katika zama za kale na kwa njia mbalimbali alinena na baba zetu kupitia manabii." Wakati Neno la Bwana lilipowajia manabii, na wao pekee, kwa sababu walitiwa upako na Neno, walikuwa na haki ya kulifasiri Neno. Naye Mungu alifanya kazi kupitia wao, akithibitisha kwamba Neno lilikuwa sahihi. "Ikiwa mimi . . . akiwepo mmoja miongoni mwenu aliye wa kiroho, ama nabii, mimi Bwana nitajifanya Mwenyewe nijulikane kwake. Na ikiwa yale asemayo yanakuja kutimia, basi

msikieni. Yasipotimia, msimsikie." Hiyo si zaidi ya hoja nzuri, kwa mtu yeyote.

51 Sasa tunajikuta wenyewe hapa, katika siku za mwisho sasa, wakati tunakutazamia Kuja kwa Bwana tena.

52 Ninamkumbuka vizuri maskini mhubiri wa Kibaptisti aliyenibatiza katika Jina la Yesu Kristo, nilipokuwa mvulana mdogo tu. Na alikuwa akijadili jambo hili na mimi, kuhusu Yohana Mbatizaji. Alisema, "Ndugu Billy," akasema, "wakati Yohana . . . Wakati Yeye aliposema, 'Kubali iwe hivyo,' na halafu akamruhusu." Akasema, "Ndipo Yohana, akabatiza . . . Yesu akambatiza Yohana, kwa sababu tunajua Yohana hakuwa amewahi kubatizwa, na hata hivyo alikuwa akihubiri ubatizo." Vema, hilo daima kwa namna fulani lilinifadhaisha, kidogo.

53 Ndipo hapa si muda mrefu uliopita, lilifunuliwa kwangu, namna hii, kwamba pale walikutana kwenye kile kidimbwi, katika lile shimo la maji, wajumbe wawili mashuhuri kuliko wote ulimwengu uliowahi kuona: m—mtu aliyekuwa juu ya manabii wote, ambaye alikuwa ni Yohana, "hakukuwahi kuwa na mtu aliyezaliwa na mwanamke, mkuu kama alivyo yeye"; na hapo alikuwepo Mungu, Mwenyewe, amedhihirishwa katika mwili wa nyama. Pia kumbuka, na Biblia inatwambia kwamba, "Neno la Bwana humjia nabii." Basi wakati Neno lilipofanyika mwili; huyu hapa alisimama nabii ndani ya maji. Ndipo Neno na nabii wakakutana, walijuana! Kweli. Neno Lenyewe, lililofanyika mwili, Mwana wa Mungu aliyechukua mwili, alimjia nabii, ndani ya maji.

54 Nabii akasema, "Nina haja kubatizwa na Wewe, basi kwa nini Wewe waja kwangu?"

55 Akasema, "Kubali hilo hivyo, kwa kuwa yatupasa kwamba tutimize haki yote."

56 Angalia! Yohana, akiwa nabii, alijua kwamba Yeye alikuwa ni Dhabihu. Na dhabihu haina budi kuoshwa kabla haijatolewa kwa ajili ya sadaka. Na hiyo ndiyo sababu ilibidi Yeye abatizwe.

57 Loo, leo hii, inatupasa sisi, kwamba tutimize haki yote ya siku yetu. Saa imewadia. Biblia inatuambia kile kinachopaswa kuwa kikifanyika katika siku hii. Tunajua kile Biblia isemacho kitatendeka katika siku hii. Ni juu yetu kumshikilia Mungu mpaka mambo haya yafanyike. Hii ndiyo saa! Ombeni kwa ajili ya mpakwa mafuta atakayetupatia ukombozi tunaoutafuta, kwa sababu Mungu ameuahidi.

58 Walilikataa Neno la Mungu lililopakwa mafuta wakati ule, na kwa hiyo ukaanguka, ukaporomoka. Na tena tunaona, kwenye wakati huu, pia unaporomoka tena. Ninaona, kama nilivyosema, siasa zetu zimeoza, maisha yetu ya kanisa yameoza. Ni nini kilichofanyika? Hiki hapa kilichofanya hayo; ukiondoka kwenye, wakati wowote, kutoka kwenye mpango wa Mungu,

utapata uozo. Hauwezi kusimama. Neno la Mungu halikosei, na hakuna kitu kingine kitachukua mahali Pake, kamwe hakiwezi.

59 Mfumo wetu wa elimu, mfumo wetu wa kidhehebu, umechukua mahali pa Roho Mtakatifu kuongoza kanisani. Mafunzo yetu mashuhuri ya wahudumu na kadhalika yamechukua mahali pa—pa mikutano ya maombi ya usiku kucha, na njia ya kale tuliyokuwa tukimwendea Mungu. Sasa, badala ya kuwa na wahubiri, tuna wahutubu, watu wanaojua Neno vizuri, wanaweza kukaa hapo na kuweka Hilo pamoja kwa njia ambayo linashangaza jinsi wanavyoweza kufanya hilo. Wanajua mitambo, bali hiyo siyo Nguvu tendaji. Tunataka Nguvu tendaji. Sijali kuhusu mitambo; ninataka kujua Nguvu tendaji. Hizo hufanya nini?

60 Sijui jinsi motokaa hiyo hukimbia huko nje. Inazo pistoni na silinda, nami sijui ni presha kiasi gani iliyotumia. Kitu pekee nijuacho ni nguvu tendaji, iweke huko nje na uiendeshe.

61 Hicho ndicho tujuacho, Mungu alitoa ahadi, "Nitamwaga Roho Yangu juu ya wote wenye mwili, wana na binti zenu watatabiri." Yeye anaendaje kufanya hilo? Siwezi kukuambia. Ninataka tu kujua Nguvu tendaji za mfumo wa Mungu. Hicho ndicho kitu kikuu.

62 Leo hii tumejifunza mitambo mpaka yote ni ya kimitambo. Motokaa inafaa nini bila ya kitu ndani yake kuiendesha? Taa zinafaa nini kama—kama . . . ama nyaya, kama hakuna umeme wa kuzipitia? Unaona, tunayo mitambo yote, tunazo shule na waelimishaji, na kadhalika, wanaoweza kumfunza mtu, mpaka anaweza kusimama mimbarani akiwa na adabu sana mpaka yeye ni msemaji hodari. Hiyo bado haileti Nguvu za Mungu. Ziko wapi Nguvu za Mungu zilizokuwa kanisani? Iko wapi ile Baraka ya kipentekoste iliyokuwa ikitembea kupitia makanisani? Hiyo ndiyo sababu ulimwengu wetu unaporomoka, kwa sababu tumeondoka kwenye kanuni hasa za Mungu, na kuwaelimisha watu katika mifumo na kadhalika. Na hiyo ndiyo iliyotuingiza katika hali tuliyomo leo hii. Ninaamini hiyo ndiyo sababu ulimwengu wetu unaporomoka.

63 Visa hivi vimekuwapo duniani tangu siku za Nuhu. Tunaona wakati ninii ya Mungu . . . alikuwa na Nuhu, nabii wa haki, akienenda na ujumbe wake, kulikuwa na kisa cha utovu wa uadilifu katika siku hiyo, kama Biblia ilivyosema, "Wakila, wakinywa, wakioa, wakiolewa." Tunaona, ulafi na utovu wa uadilifu, na kadhalika, zilifanyika siku hiyo. Ndipo basi ulimwengu uliporomoka kwa sababu watu waliukataa ujumbe wa Mungu, kwa ajili ya siku hiyo. Nuhu alikuwa nabii aliyepakwa mafuta na Mungu, aliyetumwa na Mungu, na ujumbe kutoka kwa Mungu, naye aliwapa watu onyo kabla ya hukumu kuja. Na wao walibeza na kucheka, na kuudhihaki, na kukejeli, nao mfumo wote wa ulimwengu ukaporomoka, katika siku hiyo,

nao wakazamishwa chini ya bahari. Hiyo ni kweli. Kwa nini? Waliukataa ujumbe wa wakati.

64 Tunaona jambo lilo hilo lilitokea huko Misri, wakati Musa alipowaongoza watoto wa Israeli kutoka. Mfumo wote wa Misri ulikuwa umeoza. Na tunaona sasa ilitukia tena, wakati Mungu alipomtuma mjumbe aliyepakwa mafuta huko chini kwa ajili ya Neno Lake. Ilikuwa ni kutimiza Neno Lake.

Unasema, "Je! ilikuwa ni kutimiza Neno Lake?"

65 Alimwambia Ibrahimu hilo ndilo hasa Yeye angefanya. Na ilibidi pawe na mtu anayekuja jukwaani, kwenye wakati huo, kulifanya Neno hilo liishi moja kwa moja mbele yao. Mungu alikuwa amemtuma Musa Wake huko chini, na, kitu hasa Yeye alichoahidi kufanya, alikifanya, kwa sababu yeye alikuwa ndiye Neno lililopakwa mafuta kwa ajili ya wakati huo. Alisema lingeuhukumu ulimwengu huo. Neno la Mungu lilisema, "Nitalihukumu taifa hilo kwa maajabu makubwa yenye nguvu, na ishara.

66 Hapo alisimama mtu, mtu tu wa kawaida kama wewe au mimi, aliyekuwa na Neno kutoka kwa Mungu, na akaenda huko nje na kunena maumbile yakawepo. Kasema, "Hebu. . . " Akachukua mchanga, na kusema, "Viroboto na viwepo kutoka ardhini." Na Neno la Mungu, kupitia kinywa cha nabii huyo, kwa kuwa ilikuwa moja kwa moja katika wakati lilipopaswa kuwa, viroboto vikaijaza nchi nzima. Akaijaza nchi na vyura, na chawa. Aliijaza na kila namna ya—ya tauni na kadhalika. Kwa sababu, Mungu alitoa ahadi, na saa ilikuwa imewadia kwake kutiwa mafuta, Neno lililopakwa mafuta kwa saa hiyo wanayoishi.

67 Hicho ndicho tunachohitaji leo hii, si nyuma katika mfumo fulani wa kiseminari, bali Neno lililopakwa mafuta kwa ajili ya saa tunayoishi, kumleta Yesu Kristo kwa ulimwengu tena. "Yeye yule jana, leo, na hata milele." Kuna—kuna mpango uliowekwa kwa ajili ya siku hii, ahadi ya Mungu. Na njia ya pekee ya sisi kuweza kuwa sahihi, ni kuliacha hilo Neno lipakwe mafuta. Hiyo ni kweli. Imefanyika daima. Naam.

68 Tunaona ule mchafuko mkubwa wa kimaadili katika siku za Nebkadreza. Yeye alikuwa na mtu aliyepakwa mafuta. Wakati maandishi ya mkono yalipokuja ukutani, Yeye alikuwa na mtu aliyeweza kuyasoma.

69 Siku za Lutu na Sodoma, tunaona tena ulimwengu ukiporomoka. Mungu aliokoa kile kilichoweza kuokolewa, kutoka kwake.

70 Katika siku za Yesu Kristo, tunaona kwamba mifumo iliyobuniwa na wanadamu ilikuwa imeingiza ulimwengu katika hali kama hiyo, na siasa zao za siku hiyo, mpaka, wao, ulimwengu wote ulikuwa unaporomoka, kwenye Krismasi ya kwanza.

71 Sasa tumefanya jambo lile lile, tumegeuka moja kwa moja tukazunguka tena na kulipotosha Neno la Mungu, kwa dini ya kimfumo, mpaka tunauona ukiporomoka. Ni upi mmoja kati ya mifumo hiyo tunaoweza kutegemea sasa? Ni mfumo gani tunaoweza kuendea, mfumo wa Methodisti, Baptisti, Presbiteri, au wa Kipentekoste? Hakuna kitu hata kidogo tuwezacho kufanya ila kurudi kwenye Neno hilo lililopakwa mafuta la ahadi ya wakati huu. Mifumo hii ni dhaifu, inapepesuka. Hiyo, hiyo ni, hiyo ni mifumo iliyobuniwa na wanadamu, nayo haitakuokoa. Hakuna Uzima ndani yake. Uzima umo tu ndani ya Neno la Mungu. Ni Uzima. Yeye alisema hivyo.

72 Na jinsi ilivyokuwa wakati ule, kama walivyokuwa wakiomba, watu hujikuta katika mwisho wa safari yao, au mwisho wa kamba zao, kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu na siku za Musa, na kadhalika. Wakati wanapojikuta, kwamba hawawezi kuendelea zaidi, ndipo wanaanza kuomba. Na wakati wakianza kuomba, Mungu daima hujibu. Ndipo Yesu akazaliwa.

73 Ulimwengu kwenye wakati huo, kama nilivyosema, ulikuwa unaporomoka. Kila taifa lilikuwa linamtazamia masihi, kama tu tulivyo leo hii. Rumi ilikuwa ikitazamia mtu mashuhuri mwenye kipaji ambaye angeweza kuja miongoni mwao, ja—jamaa mashuhuri aliyekuwa na ujanja wote wa kijeshi, hata angeweza kwenda huko na kukanyagia mbali Ugiriki na ulimwengu wote. Ugiriki ulikuwa unatazamia kitu kile kile, mtu fulani ambaye angeweza kuwaambia jinsi ambavyo wangeweza kuuteka ulimwengu wote.

74 Ulimwengu wa kidini wa Kiyahudi wa siku hiyo ulikuwa ukimtazamia jemadari. Walifikiria angekuja Masihi ashuke kutoka Mbinguni, akiwa na fimbo kubwa ya chuma mikononi mwake, na Yeye angeipiga Rumi, awakanyagie mbali na kuwafukuza hadi baharini. Na wote kule, walikuwa wakitazamia mtu wa namna hiyo. Walitaka jemadari.

75 Kama vile sana kama madhehebu yetu ya leo hii, madhehebu yetu yanatazamia mtu mwenye uwezo kupita kiasi. Taifa letu linatazamia mtu mwenye uwezo kupita kiasi. Urusi inatazamia mtu mwenye uwezo kupita kiasi. Ulimwengu wa mashariki unatazamia mmoja. U.N. unatazamia mmoja. Makanisa yanatazamia mmoja. Lakini ni wa aina gani wanayemtazamia?

76 Urusi inamtazamia masihi aliyepakwa mafuta mwenye—mwenye akili hata anajua jinsi ya kuteka anga za nje kwa ajili yao, apige kila mtu hadi kwenye mwezi. Wanataka kuuteka ulimwengu. Hiyo ni ninii tu . . .

77 Lakini, unaona, wanapoomba mambo haya, na kuomba kwa ajili ya hili, hawaombi kama Yesu alivyosema. Tunajaribu kumfanya Mungu kama—kama tarishi, "Bwana, Wewe nifanyie *hili*! Na Wewe nifanyie *hili*! Na Wewe nenda ufanye *lile*," kumwambia Yeye jambo la kufanya.

78 Yesu alisema, "Mwombapo, ombeni hivi, 'Baba Yetu Uliye Mbinguni, Jina Lako litukuzwe. Ufalme Wako uje. Mapenzi Yako yafanyike.'" Ambaye, unaona mahali tunafanya hilo? Daima tunamtaka Mungu kutufanyia kazi zetu, ama kutufanyia jambo fulani. Lakini tukiwa tayari kusema, "Mapenzi Yako yafanyike," kujikabidhi Kwake, kuzikabidhi njia zetu Kwake. Yote tuliyo, tuyakabidhi Kwake. Hapo ndipo Mungu atakaposogea, wakati ukiwa tayari kumruhusu Yeye afanye kazi juu yako, si wewe kufanya kazi juu Yake.

79 Acha Yeye akwambie, si wewe kumwambia Yeye na kulipindua. "Njoo kwenye mfumo wetu, Ee Bwana Mungu, tufanye sote Methodisti, sote Pentekoste, tuwatawale hao wengine. Tunataka mwenye kipaji kikubwa, sisi watu wa Kipentekoste, sisi Methodisti na Baptisti." Tunazo seminari, tunajenga kubwa kubwa, mkisema, "M—mwisho wa wakati umekaribia, kule Kuja kwa Bwana," mkijenga seminari zenye gharama ya mamilioni ya dola, na kadhalika. Mkijaribu kufanya nini? Kutupatia masihi. Hiyo ni kweli.

80 Acha Bwana ainue kitu fulani nje mahali fulani, kila dhehebu hujipatia kimoja cha namna hiyo. Hiyo ni hakika. Chunguza. Angalia wakati uponyaji wa Kiungu ulipoanza, ni waponyaji wangapi wa Kiungu? Ilibidi kila mtu kuwa mponyaji wa Kiungu.

81 Kulikuwa na Musa mmoja katika siku za kule kutoka. Kulikuwa na Eliya mmoja, Elisha mmoja, Isaya mmoja, na kadhalika.

82 Sasa tunaona kwamba ulimwengu unataka masihi wao wenyewe. Urusi inataka wao, na Marekani inataka wao, ulimwengu wa kanisa unataka wao. Kila mmoja wanataka masihi wao wenyewe, lakini wanalitaka katika njia ambayo—ambayo wao wanaweza kulidhibiti. Wanataka kuwa na udhibiti juu ya huyu masihi. Loo, hakika. Naam, wao, kama wangeweza kumpata. Kama Mungu angemtuma kwa ladha yao wenyewe, hakika wangemkubali. Lakini unaona, basi, Mungu alijua mahitaji yao. Yeye, Yeye hajaahidi kututumia matakwa yetu na kile tunachoomba, bali mahitaji yetu.

83 Walitaka jemadari; wakampata Mtoto mchanga. Unaona, hicho ndicho walichohitaji. Walihitaji mtoto mchanga (kitu gani?) kuwashushia hadhi, kuwanyenyekeza.

84 Hilo ndilo kanisa la mtindo wake linalohitaji leo hii, kujinyenyekeza tena. Wamefikia mahali, hamna maungamo wala hakuna upendano miongoni mwa watu. Inaonekana kana kwamba unakufa kila siku. Kanisa linaingia baridi. Kila mahali, unakuta uamsho umeisha, na unakuta hali ya baridi ikiingia. Tunahitaji kushushwa hadhi. Na sisi . . .

85 Waliomba wapewe jemadari; wakapata Mwana-kondoo. Kwa nini? Hiyo ni, Mungu alijua kile walichohitaji. Hicho

ndicho walichohitaji. Walihitaji Mwokozi. Walidhani walikuwa wameokoka, lakini Mungu alijua hawakuokoka.

86 Na hicho ndicho ulimwengu unachohitaji leo, tena, ni Mwokozi, Mwokozi wa hali hii, kitu fulani kinachoweza kuushikilia pamoja. Si enzi ya elimu, namna fulani ya mfumo wa kimtindo, ama namna fulani ya mfumo wa elimu. Tunachohitaji ni Nguvu za Bwana Yesu Kristo, na neema iokoayo, kurudi kanisani tena, wakati wanaume, wanawake, wavulana, na wasichana, wanaweza kuokolewa.

87 Hivi tumengoja muda mrefu kupindukia? Je! wako wengi nje ambao kamwe hawataingia? Je! jina la mwisho limekombolewa? Je! hiyo ndiyo shida leo hii? Huenda ikawa, mnajua. Mnajua, i—inawezekana kwa urahisi kuwa hivyo, na kamwe isivuruge Maandiko, hata kidogo. Huenda ikawa. Kwa hiyo, sisi hatujui sasa, hebu tujihadhari.

88 Lakini walidhania kwamba waliokoka, na—na, bali Mungu alijua vema kuliko walivyojua. Na jambo lilo hilo hufanyika leo.

89 Walikuwa wamechukua Neno ambalo Mungu alikuwa amewapa kwa ajili ya siku hiyo, hata walipaswa kuwa wamejua siku ambayo Yeye alikuwa anakuja, na walikuwa wamefanya desturi kutokana na Hilo. Yesu alisema, "Mmelichukua Neno la Mungu na kulitangua, kwa mapokeo yenu."

90 Hilo ni jambo lile lile ambalo limetendeka leo katika mfumo wetu, ulimwengu wa mfumo wa dini. Mifumo ya ulimwengu imelichukua Neno la Mungu na kufanya Hilo kuwa la mapokeo. Na hiyo ndiyo sababu Hilo halina nguvu zozote ndani Yake. Hakuna kitu kitakachotokana na Hilo, kwa sababu Hilo limechanganyishwa.

91 Huwezi kuweka mahindi halisi katika kitu fulani ambacho hakitaninii, isipokuwa iwe ni udongo, na hayo hayatakua. Unaweza kuyaweka kwenye jua na kuyafanya kuwa na joto, unaweza kufanya utakalo, bali unahitaji kiasi fulani cha udongo. Hayana budi kuwa mle ndani. Hayana budi kuzikwa. Lazima yawe chini ya mazingira yafaayo, kuyafanya yazae.

92 Na vivyo hivyo na Neno la Mungu! Huwezi kulichukua kanisa na kulifanya kuwa hai, juu ya mapokeo fulani. Huenda ukawaleta washiriki, mamilioni yao, bali kamwe hutashusha Nguvu za Mungu mpaka turudi kwenye Neno la asili tena, kurudi kwenye Neno la kimsingi, kurudi kwenye Damu, kurudi kwake Ye—Yesu Kristo, kurudi kwa mikutano ya maombi ya mtindo wa kale, na kurudi kwa Mungu! Huenda tumeenda kwa mbali, sasa, hata saa imepita kwa mbali. Bali, hata hivyo, Injili lazima ihubiriwe. Hatupaswi kuamua hiyo.

93 Mungu alijua walichohitaji, kwa hiyo Yeye aliwapa kile walichohitaji. Kwa hiyo tena, tunaona, kile walichokuwa nacho, tumefanya jambo lile lile.

94 Urusi na hao wengine wote wanataka wao. Nao wanasayansi mbali mbali wanataka kujitengenezea jina kubwa. Kila taifa linataka kumchukua mtu wake mwenye akili nyingi. Tunataka wetu. Tunataka mfumo wa elimu ndani yake. Tunataka umadhehebu. Hicho hakika ndicho tulicho nacho. Hicho ndicho mlichofanya. Hicho ndicho mlichotaka, hicho ndicho Mungu amewapa. Sasa mnaenda kufanya nini nacho baada ya kukipata?

95 Tunazungumza kuhusu Urusi kwa dakika nyingine. Warusi wanatafuta mtu awezaye kuteka anga. Wanawafunza upesi wawezavyo, wanasayansi wao. Vipi kama wakimpata mmoja, vipi kama wakimpata masihi wao, tunaenda kufanya nini? Basi rehema kwetu kama wakimpata! Kumbukeni, Ujerumani ilimpata tu masihi kama huyo si muda mrefu, si muda mrefu sana uliopita, Hitler. Nasi tunajua kile lilichowafanyia.

96 Sasa vipi kuhusu kanisa, ni masihi wa namna gani ambaye kanisa linamtazamia, leo hii? Nyinyi, kanisa, mmelia kwa sauti kubwa kuliko zote. Kwa hiyo, ni kitu gani tunachopigia makelele kuhusu masihi, ni kwa nini tunapiga makelele? "Uamsho katika wakati wetu! Rudi *hili*, *lile*, na *linginelo*." Wanatazamia nini, kufanya hilo? Ni nini zaidi mnachotaka? Kanisa linataka nini, hata hivyo?

97 Tayari tumelipata Hilo! Mungu alitupa Hilo. Ni ahadi Yake kwa ajili ya saa hii. Tunaangalia katika Biblia, tunaiona kila mahali katika Biblia. Waliopakwa mafuta walikuja na kulifanya hilo Neno kuishi tena, moja kwa moja katika majira kwa ajili ya saa hiyo. Nasi tumempata Masihi. Huyu ni Yeye, Neno! "Hapo mwanzo alikuwako Neno, naye Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu." Na Neno linabaki Mungu, Waebrania 13:8, "Yeye yule jana, leo, na hata milele." Tunajua kile kinachopaswa kutokea katika siku hii. Tunamtaka Masihi. Naye Mungu alitupatia Masihi, Neno Lake lililoahidiwa kwa ajili ya siku hii. Linangojea tu mtu fulani aliye na imani, kulitia Hilo upako na kulifanya liishi tena. Naam, bwana. Hilo ni Masihi halisi, Hilo ni Neno la Mungu. Ambalo, Yesu alisema, "Mbingu na nchi zote zitapita, bali Neno Langu halitapita kamwe."

98 Bali kanisa limeketi limekufa kiroho, limekwisha, wakati umewapita. Wako katika usingizi, na hata hawajui la kufanya, mmoja anakimbia *huku* na mmoja *kule*. Na hapa kila ahadi ambayo Mungu alifanya katika Biblia, kila mojawapo, ipo hapo ikiwa nzuri tu kama zilivyowahi kuwa. Huu ndio wakati! Ni kitu gani kinachofanya kanisa namna hii? Tuko katika wakati wa Laodikia, wakati inambidi kuja namna hii. Huu ndio wakati kwa ajili yake.

99 Lakini kumbukeni, humo ndani mna wakati ambapo bikira aliyelala alikuja kununua Mafuta, na huo ulikuwa ndio wakati ambapo Bwana-arusi alikuja. Tunaona leo, Waespiskopolia,

Presbiteri, na madhehebu mbalimbali, ambayo, miaka michache iliyopita, usingeweza kuwakodi kuenda karibu na kundi la waaminio wa Kipentekoste. Sivyo hakika. Lakini wao hapo, leo hii, wanaingia. Hivi hamjui kile Yesu alichosema? Walikuja kununua Mafuta, na kusema, "Tupeni Mafuta yenu kidogo." Wale waliokuwa na Mafuta, wakasema, "Sivyo. Nendeni mkanunue, la sivyo...kutoka kwa hao wanaouza Hayo." Ndipo wakati walipokuwa wakijaribu kununua Hayo, wakati walipokuwa wakijaribu kupata Hayo! Je! mnajua ni wakati gani tunaoishi, enyi watu wa Kipentekoste? Wakati walipokuja, huenda walichanganyikiwa, huenda walifanya *hili*, *lile*, ama *linginelo*; bali, kulingana na Maandiko, hawakuyapata Hayo. Wakati walipokuwa wakijaribu kufanya hilo, huenda walipitia misisimko yote, na kisha itikadi zote na mihemko, lakini ibilisi anaweza kuiga mambo hayo yote. Wakati walipokuwa wakinunua Hayo, ama kujaribu kutafuta Hayo, Bwana-arusi akaja, na wale waliokuwa na Mafuta wakaingia ndani.

100 Na hiyo hapo saa tunayoishi. Hatujawahi kuiona hapo kabla. Yesu alisema itakuwa hivyo, basi ni hivyo! Tunaona kitu gani? Tunaliona Neno, ambalo Mungu alisema litatokea katika siku hii, likitokea moja kwa moja chini ya nyuso zetu. "Loo, basi amkeni, enyi watakatifu wa Bwana, kwa nini msinzie wakati mwisho unakaribia; hebu tujiweke tayari kwa ajili ya ule wito wa mwisho," kwa kuwa hatujui utakuwa lini. Naam.

101 Mfumo wetu wa ulimwengu, mfumo wetu wa kanisa, mfumo wetu wa kimadhehebu, mifumo yetu yote, imechafuka na kuoza. Tulichokosa leo ndicho walichokuwa nacho jana. Hiyo ni kweli. Inaonekana kama ni kukauka, kwa makanisa, ni vigumu kuweza kupata kanisa tena ambalo liko hai likiwa na Neno na likiwa na Roho wa Mungu, na mambo makuu yakitendeka kama ilivyokuwa muda si mrefu uliopita.

102 Sasa, tunaona kwamba Mungu anajua kile walichohitaji, kwa hiyo Yeye—Yeye daima hujibu ahadi. Ni Neno hili kuu tu tunaloona, ahadi, walipaswa kujua kwamba lilikuwa hasa kile Mungu alichoahidi, kwamba kingetukia katika siku hiyo.

Unasema, "Vipi, ni kitu gani kilikuwa kitendeke?"

103 Isaya 9:6, nabii alisema, "Kwetu amezaliwa Mtoto, Mwana, Mtoto; Mwana amezaliwa, tumepewa Mtoto: na Jina Lake litaitwa 'Mshauri, Mfalme wa Amani, Mungu Mwenye Nguvu, Baba wa Milele'; na utawala utakuwa mabegani Mwake, na Ufalme Wake hautakuwa na mwisho."

104 Tunajua kwamba tulipaswa kuwa na Mtoto akizaliwa katika siku hiyo, bikira anapaswa kuchukua mimba na kuzaa Mtoto. Na Huyo hakuja kupitia mfumo wao wowote, kwa hiyo hawakutaka uhusiano wowote na Yeye. Walimkataa Huyo. Bali Neno lililopakwa mafuta, Mungu (Imanueli) aliyefanyika mwili miongoni mwao, alisimama hapo, Yeye akasema, "Ni nani kati

yenu awezaye kunihukumu kwamba nina dhambi, kutokuamini? Yachunguzeni Maandiko, kwa kuwa ndani yake mnadhani mna Uzima wa Milele, na hayo ndiyo yanayonishuhudia Mimi." Alitambulishwa kikamilifu kwamba Yeye alikuwa Masihi, Masihi aliyepaswa kutokea katika siku hiyo. Nayo mifumo ilikuwa—ilikuwa imevuruga akili za watu, katika sheria nyingi sana za kimifumo, na kadhalika, hata walikuwa wamelitangua Neno la Mungu. Wasingeweza kuona Yeye alikuwa ndiye Masihi.

105 Na kama ilivyofanya wakati ule, ndivyo imefanya tena. Kweli. Mifumo ya ulimwengu, mitambo, imeweka pistoni mahali ninii—mahali bomba la ekzosi linapaswa kuwa, katika mitambo yao mikubwa. Na kwa hiyo inawezaje kukimbia? Haiwezi. Haikujengwa namna hiyo.

106 Kanisa haliwezi kuenenda bila ya Nguvu za Mungu, kupitia Neno. Naye Roho Mtakatifu atathibitisha tu Neno la Mungu, kwa kuwa hiyo ndiyo anayopaswa kufanya. Upako unapaswa kulithibitisha Neno.

107 Na Yesu alikuwa Ndiye Mtiwa Mafuta, Neno lililofanyika mwili. Hiyo ndiyo sababu Yeye alitembea akaingia majini kule, Yeye alikuwa ni Neno likija kwa nabii. Alibatizwa na nabii. Ndipo basi nabii akasimama, na kusema, "Lazima nipungue; Yeye atazidi." Tunaona kwamba hiyo ndiyo njia ya Mungu ya kulifanya.

108 Lakini je! walilipokea Hilo? Walipaswa kujua Hilo. Walipaswa wawe wameangalia matendo ya Mungu. Waliliona Neno likitimia. Walijua Maandiko yalisema hivyo, bali wasingeweza kuamini Hilo lingekuja namna hiyo. Ilibidi lije ama kwa Mafarisayo au Masadukayo. Kama lingekuja kwa Mafarisayo, Masadukayo wasingalilipokea Hilo. Vinginevyo, Ma—Masadukayo wasingeweza kupokea Hilo, kwa sababu walisema Mafarisayo wangekuwa Nalo.

109 Na hivyo tu ndivyo ilivyo leo hii, mifumo yetu, na kitu chote kilikuwa kimeoza na kuchafuka. Loo, jamani! Saa tunayoishi sasa, ulimwengu uliopofuka, unaotembea katika giza, uliozama katika mifumo ya ulimwengu huu, kama kondoo bila mchungaji. Wakati wamekuwa na Neno la Mungu aliye hai likithibitishwa mbele zao, na kuondoka kipofu, na kuacha Hilo, unawezaje kutarajia kitu kingine? Amina. Tupo hapo.

110 Basi, ulimwengu unaporomoka. Kwa nini? Neno lenyewe lililoushikilia pamoja limekataliwa. Tunapata hilo katika Waebrania, mlango wa 11.

111 Einstein alisema. Nilikuwa nikisikiliza hotuba yake, hapa hivi majuzi usiku, Mji wa New York, aliyotoa moja ya hotuba zake za mwisho. Alikuwa akizungumza kuhusu mkusanyiko, galaksi ndogo, ilikuwa, nje katika mkusanyiko. Akasema, "Kama mtu angeanza kupitia angani, akisafiri katika mwendo wa nuru..." Ni nini hiyo, elfu nane...[Mtu

fulani anasema, “Mia moja themanini na sita elfu.”—Mh.] Maili mia moja themanini na sita elfu kwa sekunde moja. “Ingemchukua mia moja, ingemchukua miaka milioni mia moja na hamsini ya nuru kufika kule.” Alipata Umilele. Ndipo kasema, “Kurudi, ingemchukua miaka mingine milioni mia moja na hamsini, ambayo ingekuwa miaka milioni mia tatu. Na kipindi, alichokuwa ameondoka duniani, kingekuwa tu miaka hamsini.” Haya basi, akapenya kuingia Umilele! Loo, jamani! Ukuu wa Mungu, wakati Yeye alipoumba mfumo wote wa jua!

112 Basi huyu mwanaanga, hivi majuzi, akiruka huku juu ya Urusi kule, na kusema yeye “hakuona Mungu yeyote, Malaika.” Watu wanawezaje kuwa wasiojua! Wakati . . .

113 Mungu! Na mfumo wote wa jua, Yeye aliupuliza kutoka kwa mikono Yake; na Yeye anaketi miaka milioni nyingi sana, miaka ya nuru, zaidi ya hiyo. Na kitu chote kimeshikiliwa na Nguvu Zake na Neno Lake. Haleluya! Kila nyota haina budi kuning’inia mahali pake. Naam, bwana! Halafu, alikuwa mnyenyekevu vya kutosha kushuka na kufanyika mmoja wetu, kufa kwa ajili yetu; hatuna udhuru. Kama moja ya nyota hizo ingetokea kuwa isonge kutoka kwenye soketi zake, kutoka kwenye mzingo wake mahali ilipo, kama hiyo ingesonga, ingevuruga mfumo wote. Mfumo wote lazima upinduke vile vile, kwani moja inategemea nyingine.

114 Na mfumo wa Mungu, wakati ukiwa katika uwiano mkamilifu na Yeye, kitu hicho chote hufanya kazi kikamilifu. Hiyo ni kweli, kwa sababu inabidi iwe hivyo.

115 Lakini kanisa kamwe halikuchukua mfumo wa Mungu, lilijiundia mfumo wake lenyewe. Hiyo ndiyo sababu sisi sote tuko nje ya uwiano. Hiyo ndiyo sababu kanisa limevurugika kabisa. Hiyo ndiyo sababu ulimwengu unaporomoka leo hii, kwa sababu tumechukua mifumo yetu wenyewe. Hiyo ndiyo sababu ulimwengu wa siasa umesambaratika. Hiyo ndiyo sababu ulimwengu wa kidini umeporomoka, ni kwa sababu tumechukua mfumo badala ya kuchukua mpango wa Milele wa Mungu kwa ajili ya nyakati. Amina. Hiyo ndiyo shida ya ulimwengu. Hiyo hasa ndiyo kasoro, ni kwa sababu wamechukua kitu kingine. Imewashika watu sana, “Mimi ni Presbiteri. Mimi ni Methodisti. Mimi ni Umoja. Mimi ni Utatu. Mimi . . . ” Loo, rehema! Si ajabu hatuwezi kushikana pamoja, hakuna kitu cha kutushikilia pamoja.

116 Bw. Nixon alitoa tamshi la busara kuliko yote niliyosikia rais yeyote au makamu wa rais akitoa katika miaka michache iliyopita, wakati aliposema hivi majuzi, “Watu wa Amerika wana shida gani, wamepoteza upendo na heshima mmoja kwa mwingine.” Kama wananchi wa Marekani tukipigana risasi na kuangushana, barabarani, tunawezaje! Jamani!

117 Ikiwa huwezi kutofautiana na mtu, na kumpenda wakati uo huo, basi nyamaza. Kama huwezi kumwambia, kama baba akimrekebisha mtoto wake, kwa mkono ulio tayari kuuweka shingoni mwake na kumkumbatia baadaye, heri uachane nalo. Hujaenda mbali vya kutosha, wewe mwenyewe, kujua kile unachozungumzia. Kweli. Ninaweza kutofautiana na mtu, hakika; angali ni ndugu yangu, nitaushika mkono wake. Siwezi kumwacha aende na hiyo; kama nikifanya hivyo, kama sikumwambia, nisingekuwa ndugu sahihi kwake. Hiyo ni kweli. Bali ninaweza kumwambia, na kumwambia ninampenda, na kumthibitishia, ninampenda.

118 Haikubidi kumpiga risasi na kumwangusha, barabarani. Ninatofautiana na Bw. Kennedy na—na siasa zake, na dini yake, na kadhalika, lakini hakustahili hayo. La, bwana. La, hasha. Hakuna mtu anayestahili hayo.

119 Kwa hiyo, tunakuta kwamba ulimwengu wote umeoza. Taifa letu, siasa, mifumo ya kidini, na kila kitu, kimeoza.

120 Unangojea tu. Neno la Mungu, ambalo lilitabiriwa kwa ajili ya siku hii, linangojea mtu fulani aje na athibitishe Hilo. Sijui kama Yeye tayari amefanya hilo? Basi tuko wapi basi kama Yeye alikuwa amelifanya? Kama Yeye amelifanya, basi tuko wapi? Wenye mashaka kuliko wote!

121 Nilisema jambo gumu kuhusu Bibi Kennedy, mara kadhaa, kuhusu yeye kuweka mitindo kwa ajili ya ulimwengu, na hii mitindo ya kukata nywele kichwa-maji, na, "Jinsi dada zetu na wengine hukata nywele zao, na kuvalia kama Bibi Kennedy," nikasema, "kama Yezebeli wa kale." Hiyo ni kweli. Ninaamini hilo. Ni—ni—ninamsikitikia maskini yule mama pale usiku wa leo, na watoto wake, hakika.

122 Lakini hebu niwaulizeni jambo fulani. Iwapo Jacqueline Kennedy angesikia Jumbe ambazo baadhi yenu Wapentekoste mmesikia, kuhusu kunyoa nywele zenu na kadhalika, huenda hata asingenyoa nywele zake. Mnadhaniwa kuwa wapentekoste, na mngali mnanyoa! A-ha. A-ha. Huenda asifanye hivyo kama angepata fursa na kusikia Ujumbe, mnaona, nyinyi mmesikia. Haya basi. Tuko mahali pabaya, jamani. Hiyo ni kweli kabisa. Naam, hakika. Ee Mungu, jinsi ambavyo maadili, jambo . . .

123 Tabia za wanawake ni mojawapo ya mambo ambayo hushikilia nchi yetu pamoja. Ni uti wa mgongo. Na uwanamke, sifa nzuri ambayo Mungu alimpa mwanamke kuwa mama, mbona, i—i—imekwisha. Kitambo sana wa—wa—wa—wanawake wa ulimwengu huu, sifa yao, imesujudia mungu mke wa mtindo wa Hollywood; wakijifananisha wenyewe, na kujivika wenyewe, na kutenda kama baadhi ya hawa nyota wa Hollywood wafanyavyo. Na mara nyingi ambapo hata kuvalia kwa njia isiyo ya kiungu, kuvutia kimapenzi, kunachukuliwa kama mitindo makanisani. Nao wachungaji nyuma ya mimbara, bila ya—bila

ya ujasiri, bila ya—ya uweza wa Roho Mtakatifu; kama Lutu aliyeketi kule chini, ikihuzunisha nafsi yake, na akiwa sana katika tikiti ya posho asiweze kuwaambia watu kwamba ni kosa. Naam.

124 Tunachohitaji leo hii ni kung'olewa. Huenda tukang'oa tukiwa tumechelewa mno sasa. Wakati huenda umepita. Kamwe hatuna uamsho mwingine. Ninajua mnautazamia, ila siuoni katika Maandiko.

125 Ninatazamia Unyakuo, kwa ajili ya watu wachache tu. Hiyo ni kweli, watu wachache tu. Hawatajulikana kuwa hawako ulimwenguni. Watakapokwenda, hamtajua kwamba umetukia. Hiyo ni kweli. Utakuja kama mwizi usiku.

126 Na Yeye asipofupisha kazi, kwa ajili ya Wateule! Wapo wengine waliochaguliwa kwa Uzima wa Milele, tunajua hilo; wote wako hivyo, walio na Uzima wa Milele. Na ikiwa wao—na ikiwa wao. . .ama basi Yeye haifupishi, kwa ajili yao, hakuna mwili utakaookolewa. Ulimwengu umepata maangamizi yake, kila miaka elfu mbili. Tunajua mfumo umeporomoka. Uliporomoka katika siku za Nuhu. Siku za Kristo, uliporomoka. Na hapa ni 1964 unaokuja, unabakisha nini? Miaka thelathini na sita kufikia elfu mbili nyingine; ya ishirini na moja, karne ya ishirini na moja inakuja. Kunafanyika nini? Kazi bado lazima ifupishwe. Yesu alisema, u—uozo wa siku hii, "Wateule wangedanganywa na wasingeokolewa, kama ingewezekana." Tupo hapo. Nayo kalenda inatwambia, kulingana na sayansi, kwamba tuko nje ya hiyo kwa yapata miaka kumi na mitano. Tuko nyuma kwenye kalenda ya Rumi, kulingana na kalenda ya Wayahudi, kwamba tuko nyuma, miaka kumi na mitano ishirini juu ya hilo.

127 Basi tuko wapi? Tunaona mataifa yakivunjika, na Israeli inaamka, ishara ambazo Biblia hii ilitabiri kwa ajili ya siku hii. Tunaona mambo ya kimitambo yakitendeka. Sasa Roho, nguvu tendaji za hilo Neno lililoahidiwa, kuingia ndani ya Kanisa Lake na kuwaongoza kuingia Kalvari huko, na kwenye Unyakuo! Basi tupo hapo.

128 Si ajabu tunaporomoka, hakuna kitu. . .Kitu chenyewe hasa kilichoumba dunia, Kitu chenyewe kiliwekwa hapa ili dunia igeukie, Kitu chenyewe ambacho mifumo na kila kitu kingine kilikuwa kizungukie, Neno hili ambalo, kwa Mungu, liliumba ulimwengu. Einstein alisema katika wake, kasema, "Kuna njia moja tu ya kueleza Maandiko. . .Njia moja tu ya kuelezea kuwepo kwa ulimwengu huu," kasema, "hiyo ni Waebrania 11, 'Kwa imani tunaelewa Neno la. . .kwa Neno la Mungu, kwamba ulimwengu uliwekwa pamoja kwa Neno la Mungu.'" Hayo tu. Hakuna mmoja awezaye kueleza jinsi inavyoning'inia hapo hewani, na jinsi inavyoweza kugeuka na kufanya saa zake ishirini na nne kuzunguka ikweta, kadhalika namna hiyo, na

kuzunguka mzingo wake, kila mahali, na kurudi mahali pale pale na kutokosa hata sekunde moja. Na kila nyota ikigeuka katika duara yake namna hiyo, na kusaidiana zinapozunguka.

129 Jinsi ambavyo huo mwezi huchungulia chini juu ya hiyo bahari! Kama huo mwezi ungalisogea kutoka mahali pake, tungalifunikwa na futi mia moja za maji, katika sekunde moja tu, ama mbili. Huo mwezi! Angalia, hata ungaliweza kuchimba shimo hapa, nyinyi watu mnaochimba mafuta, uchimbe hapa chini. Unaona jinsi pwani ilivyo mbali na wewe? Wewe chimba shimo hapa ardhini, na uangalie wakati wa jioni, jinsi mawimbi yanavyokuja, yataleta maji juu katika bomba lako, maji yako ya chumvi. Hakika. Ni kitu gani? Huo mwezi huyadhibiti, huko.

130 Ni mfumo wa Mungu. Ni mpango wa Mungu. Ni Amri ya Mungu. Lakini, tunaunda yetu wenyewe, hatutachukua Yake. Hebu tuharakishe sasa, ili kumaliza. Kama vile, ni vivyo hivyo Krismasi hii, tunaona ulimwengu wetu unaporomoka. Loo!

131 Mungu alitiwa upako, ndipo Yeye akaahidi Neno Lake. Alitutia upako kule nyuma, na Yeye akatuambia, akawaambia, "Wakati Yeye alipomtia upako Yesu Kristo. . . " Petro alisema kwenye Siku ya Pentekoste, alisema, "Yesu Kristo, Mtu aliyethibitishwa na Mungu miongoni mwenu kwa ishara na maajabu, ambayo Yeye aliyafanya miongoni mwenu; nyinyi wenyewe mnajua." Hao ni mashahidi. Pia kasema, "Baada ya ufufuo, na kadhalika, jinsi Yeye alivyokuwa amefanya! Jinsi ambavyo kwa mikono miovu mlimchukua Mfalme wa Uzima na kumsulubisha, Ambaye Mungu alimfufua; na sisi ni mashahidi." Jinsi Nikodemo alivyokuja na kusema, "Rabi, tunajua. Sisi Mafarisayo, Baraza la Sanhedrin kule juu, tunajua kwamba Wewe ni Mwalimu aliyetumwa toka kwa Mungu. Hakuna mtu angaliweza kufanya mambo hayo ufanyayo Wewe isipokuwa iwe ni ya Mungu." Walijua ahadi hiyo ilikuwa kwa ajili ya hapo, na walijua ilikuwa, ila mifumo yao iliwafunga sana mpaka hawakuweza kufanya lolote kuihusu.

132 Ndivyo ilivyo leo hii, jambo lile lile. Huwezi kulifanya, utasalimisha kadi yako ya ushirika mara ya kwanza utakapofanya hilo. Wewe shikilia tu hapo juu ya Neno la Mungu wakati fulani, uone kinachotokea; umekwisha. Hutakuwa maarufu. Utaondolewa miongoni mwao, na kila kitu kingine.

133 Loo, kama una huduma ndogo, watakushikilia kwa fedha zozote wanazoweza, wavute umati kutokana na huduma yako, wavutie fedha na kadhalika. Lakini angalia tu inapofikia kwenye Neno, waangalie jinsi wanavyorudi nyuma juu ya Hilo. Mnafikiri mtumishi wa Mungu hajui hilo? Vema, Yesu hata alijua kwamba Yudasi alikuwa miongoni Mwake. Ni kwa nini Yesu hakumwambia Yudasi jambo lolote? Sababu ile ile leo, inakubidi kungojea mpaka saa hiyo ifike kwa huo udanganyifu. Hiyo ni kweli. Waliipata. Wataipata.

134 Tazama, bali hawakutaka njia ile ambayo Yeye alikuja, ndivyo ilivyo leo hii. Makanisa basi yalitaka mifumo yao itiwe upako. Mafarisayo waliutaka mfumo wa Kifarisayo utiwe upako, Masadukayo walitaka mfumo wa Kisadukayo, Waherodia hivyo, kadhalika. Hiyo ndiyo njia leo hii. Kama wata...Kama Mungu atatuma upako, na kuwatia upako wa Umoja, loo, jamani, si watawaambia wa Uwili juu yake, ama Utatu, au chochote kile? Hivi Waassemblies si wangeambia wa Umoja juu yake? "Nilikuambia sisi tulikuwa sahihi!" Methodisti wangeambia Baptisti, "O jamani, unaona, tunaye!" Mnataka mfumo wenu utiwe upako.

135 Lakini Mungu aliahidi tu kupaka mafuta Neno Lake. Amina! Ninajua hiyo inachoma, bali hiyo ndiyo Kweli. Mungu kamwe habadiliki. Yeye hulipaka mafuta Neno Lake. Naam, bwana. Neno lililoahidiwa, lililopakwa mafuta kwa ajili ya wakati huo ndilo Mungu hupaka mafuta. Neno lililoahidiwa kwa ajili ya wakati huo!

136 Leo hii wanataka mfumo wa elimu, (kwa nini?) ili kwamba waweze kufanya lolote watakalo, na bado washikilie maungamo yao ya Mkristo. Loo, kama wana kitu fulani kikubwa, mahali unaweza kuenda na kuingia, ufuate mikondo, na kadhalika, na kutafuna chingamu, na—na kupigana mateke ubavuni; na kuondoka na kuwa na kumbi za burudani na kadhalika, ambapo nyote mnatoka nje na kucheza mpira wa vikapu na kadhalika namna hiyo. Sina chochote dhidi ya mpira wa vikapu, besiboli, kandanda, au chochote kile, ninii kubwa...kama hayo ndiyo yote aliyo mungu wako, ni mfuko mkubwa wa hewa. Lakini hebu niwaambieni, tunachohitaji leo hii ni Neno la Mungu, lililopakwa mafuta kwa ajili ya wakati huu, ambalo litazalisha Nguvu za Roho Mtakatifu tena. Naam, hiyo ni sawa, bali hiyo si ya kanisa. La, bwana. Inakubidi kujenga kitu kama hicho, kudumisha kanisa pamoja, afadhali ukiteketeze au kukitupilia nje, au kuleta kitu fulani humo ndani ambacho kitarudisha Neno tena. Na hayo ndiyo mambo ya ulimwengu, loo, kuyachanganya na Neno la Mungu, huwezi kufanya hivyo. La, bwana.

137 Naam, bwana, sasa wanataka mfumo. Ulimwengu utachukua mfumo. Sasa tunaona, kila mfumo mdogo wenyewe, kila mmoja wao anasema, "Ninataka Hilo lije kwangu. Ninataka Hilo lije kwa wangu." Loo, wananunua mashine kubwa kubwa, na kuwaelimisha wahubiri, na mambo kama hayo, na kuwatoa nje, kuwaangua, jamani, kwa elimu; mpaka, jamani, mtu anayahisi maneno yake, sarufi yake, ni mbaya sana, anachukia hata kuenda katika mimbara nyuma ya mmoja. Lakini tunachohitaji leo hii si mfumo wa elimu, si hotuba.

138 Tunachohitaji leo hii ni Injili inayoshikwa na Nguvu za Mungu, kuthibitisha Neno la wakati huu, kufikia ambapo atakuja mtu fulani ambaye atasimama na kuita nyeusi "nyeusi," na nyeupe "nyeupe," mtu fulani ambaye atasimama na kusema

Kweli, hata kama Hilo linakuchuna ngozi au linakufinyilia chini, au chochote Hilo lifanyacho. Hicho ndicho hasa kile—kile saa hii inachohitaji, leo hii.

139 Bali watu wanataka kitu fulani. Watu leo hii, wanawake, wanataka kitu gani? Wanataka wa—wa—watu, mchungaji, atakayesimama na kusema, "Yote ni sawa. Mnaweza kufanya *hili*, au kufanya *lile*. Ama, hayo yote ni sawa, hakuna chochote kibaya na *hilo*, mpenzi." Mhubiri huyo anahitaji kichapo cha Injili; kuruhusu nywele zilizonyolewa, kujipaka rangi.

La, unasema, "Hayo yana uhusiano gani na Hilo?"

140 Hivi hujui upande wako wa nje huakisi kilicho ndani? Si Biblia inasema hupaswi kufanya hilo? "Hata si jambo la kawaida kwa mwanamke kuomba namna hiyo."

141 Nanyi wanaume mnataka kitu kama hicho? Wahubiri, hamwezi kulisema, kwa sababu mtasalimisha kadi yenu ya ushirika, baraza kubwa litakutupa nje ukisema chochote juu yake. Mungu amsaidie mtu ambaye angejali zaidi kadi ya baraza au kadi ya ushirika kuliko vile angejali ubatizo wa Roho Mtakatifu, na Neno! Roho Mtakatifu, aliyeandika Biblia, anawezaje kukana kile Yeye alichoandika?

142 "Vema, siku za miujiza, loo, hatuhitaji hiyo leo hii. Uponyaji wa Kiungu, mambo haya mengine, ambayo, hakuna kitu kama hicho. Hicho ni upiga ramli, hicho ni, loo, kuwasiliana kimawazo." Ewe, maskini, uliyedunishwa, una shida gani? Tunahitaji—tunahitaji Injili, ikiwa Roho Mtakatifu yuko ndani yako!

143 Kama ningekuambia, "Uhai wa Beethoven ulikuwa ndani yangu," ningeweza kuandika muziki. Kama Beethoven aliishi ndani yangu, ningeishi maisha ya Beethoven. Kama Shakespeare alikuwa ndani yangu, ningeweza kutunga mashairi. Ningeandika tamthilia, kama Shakespeare aliishi ndani yangu.

144 Na ikiwa Yesu Kristo anaishi ndani yako, kazi alizofanya Yeye, na Neno Lake, Yeye ni Neno, litajithibitisha Lenyewe leo hii, kwa ahadi ile ile ambayo Yeye alitoa. Amina. Hilo ndilo Mungu analongojea. Hilo ndilo linaloshikilia ulimwengu, mbalimbali, linaloshikilia ulimwengu pamoja, ulimwengu wa kidini pamoja, ni Neno Lake, shikilia lolote la Neno pamoja. Naam.

145 Watu wanataka mfumo wa namna hiyo, hata hivyo. Wataupata. Tayari wako ndani yake, sasa hivi. Baraza la Makanisa Ulimwenguni litawapa hasa kile wanachotaka, kila mmoja wao pamoja. Jinsi Wapentekoste hawa wanavyoweza kuketi kwenye mikutano hii, na kuingia katika Mji wa Vatikani na kuandika barua iliyosambazwa, na kusema, "Kitu cha kiroho kuliko vyote nilichowahi kusema, nilipoketi kando ya Baba Mtakatifu Papa *Nanii*," na kuwa Mpentekoste na kujua

jinsi. . .Ni huduma ya Pentekoste iliyokufa. Kitu hicho chote kimekufa. Kimeoza. Kimekwisha! Kimerudi moja kwa moja katika Muungano wa Makanisa ambapo ndipo mahali pake. Kweli kabisa.

146 Lakini Kanisa la Mungu aliye hai, yule Bibi-arusi, anaendelea moja kwa moja vile vile tu. Na Yeye ataenda katika Unyakuo, kwa Neno, hiyo ni kweli, Neno na Neno yatakuja pamoja. Ikiwa sisi ni sehemu ya Kristo, sehemu Yake, inatubidi kuwa Neno Lake, maana Yeye ni Neno. Kweli. Naam, bwana.

147 Wamelikataa Neno la ahadi lililopakwa mafuta, la wakati huu, na Yeye daima ni Neno. Kama Mungu alitutumia Neno la ahadi, lililotiwa mafuta tena, kwa ajili ya wakati huu, katika 1946, Yeye angekuwa ni yule yule aliyekuwa wakati Yeye alipokuja hapo mwanzo, Neno lililopakwa mafuta kwa ajili ya wakati. Waebrania 13:8 inaitupa moja kwa moja pajani mwako tena, na inasema, "Ni yeye yule jana, leo, na hata milele." Hiyo ni kweli kabisa. Na sisi. . .Na Yeye angedumu na Neno la Baba lililoahidiwa kwa ajili ya wakati huu. Kama Yesu akija, Yeye angekuwa hasa kile Neno lilisema Hilo lingekuwa katika wakati huu.

148 Hicho ndicho Eliya alikuwa katika wakati wake. Hicho ndicho Musa alikuwa katika wakati wake. Hicho ndicho Nuhu alikuwa katika wakati wake. Hicho ndicho, kila mahali, kila nabii aliyewahi kuja. Nalo Ne—Neno, wakati Hilo lilipokuja katika utimilifu, Neno lote lililofanyika mwili miongoni mwetu, Hilo lilifanya hasa kile Hilo lilisema lingefanya katika wakati huo.

149 Kama Hilo likija leo hii, Yeye angekuwa hasa kabisa ni Yesu Kristo akiishi ahadi Yake ya kile Yeye aliahidi kufanya, kama tu vile Neno.

150 Yeye alikuwa ni Neno. Isaya 9:6 ni Yesu Kristo. Basi wakati Hilo lilipofanyika mwili na kukaa miongoni mwetu, liliishi hasa kabisa kile Hilo lilichofanya. Musa alisema pale, katika Kitabu cha Kutoka, "Bwana Mungu wako," au Kumbukumbu La Torati, "Bwana Mungu wako atainua nabii, mithili yangu; na itakuja kutimia, yeyote ambaye hatamsikia Huyo, atakatiliwa mbali kutoka miongoni mwa wa—watu." Ndipo wakati Yeye alipokuja, alifanya hasa kile Neno lilisema Yeye angefanya. Nao wakapata kosa Kwake, kwa sababu mifumo yao ilikuwa imekatilia mbali Hilo na kulitangua Neno la Mungu kwao. Unaona? Wasingeweza kuamini mambo kama Hayo. Wasingeweza kuamini mambo ya namna hiyo, kwa sababu wakati ulikuwa umepita, walidhania. Loo!

151 Kwa kuwa, Yeye amelithibitisha Neno Lake kuwa ni lile lile. Yeye angeweza kuthibitisha Neno leo hii, kama alivyothibitisha Hilo wakati ule. Yeye angekemea, vikali, kila mfumo wa kimadhehebu ulimwenguni, kama Yeye akija duniani leo hii.

Hilo ndilo alilofanya Yeye, mara ya kwanza. Hilo lingekuwa ndilo jambo ambalo Yeye angelishambulia. Hilo ndilo jambo hasa ambalo Yeye alilishambulia alipokuja hapo kwanza. Kama Yeye alivyofanya wakati ule, vivyo hivyo wangefanya kwa wakati huu, pia. Na Yeye alifanya wakati ule, kwa kuwa Yeye kamwe habadilishi Neno Lake. Kamwe habadilishi mfumo Wake. Ni vile vile daima, ni Neno lililotiwa upako kila wakati, kwa ajili ya wakati. Hiyo ni kweli.

152 Kwa hiyo tena, kama tunavyoliona leo hii, kama Yeye akija, mipango Yake kwa ajili ya kushikilia ulimwengu pamoja itakataliwa kama tu ilivyokuwa wakati ule.

153 Bali sikilizeni, katika kufunga, ninataka kusema hili. Hatujaahidiwa mfumo, hatujaahidiwa dhehebu, dhehebu kubwa, mpango mkubwa wa namna fulani. Bali tumeahidiwa Ufalme, Ufalme wa Milele. Amina. Hicho ndicho tulichoahidiwa, kuwa na Uzima wa Milele katika Ufalme huu wa Milele. Nayo Serikali inatawaliwa na Mfalme wa Milele, Neno Lake la Milele linatolewa kwa watu Wake walio na Uzima wa Milele. Nao watu wa Uzima wa Milele hawali vitu vya ulimwengu, bali imeandikwa, kwamba, "Mtu ataishi kwa kila Neno litokalo katika kinywa cha Mungu." Kwa hiyo wakati sote wawili sasa . . . Tunapokea Ufalme huu, na tunakuta kwamba, "Mbingu na nchi zote zitapita, bali Neno hili halitapita kamwe." Nalo Neno hili ndilo Ufalme. Hili ndilo Ufalme na Mfalme, Mfumo, Uzima, kila sehemu yake iko *Hapa* ndani.

154 Kama Mungu akiuhukumu ulimwengu Wake kwa kanisa, ni kanisa gani ambalo Yeye anaenda kuuhukumu kwalo? Ni mangapi yaliyoko? Mamia na mamia na mamia ya makanisa mbalimbali ya kimadhehebu. Kama Katoliki ni sahihi, Katoliki ipi? Kama Katoliki ya Kiyunani ni sahihi, basi ya Kirumi iko makosani. Kama ya Kirumi ni sahihi, ya Kiyunani iko makosani. Kwa hiyo, unaona, kama Methodisti ni sahihi, Baptisti iko makosani. Kama Baptisti ni sahihi, Pe—Pentekoste iko makosani. Kama Pentekoste ni sahihi, basi Presbiteri iko makosani. Unaona? Kwa hiyo nyote mngechanganyikiwa kabisa.

155 Lakini Mungu hajatuacha bila ya shahidi au ki—ki—kiwango chochote cha kusimama nacho. Hicho ni hili Neno! Yeye alisema, "Acha neno la kila mwanadamu liwe uongo, na Langu liwe Kweli." Hiyo ni kweli.

156 Kwani, "Mbingu na nchi zote zitapita." Tunaambiwa hapa, kwamba, "Tunapokea Ufalme usioweza kutikisika." Naam, bwana. Wakati falme hizi zote za ulimwenguni zinapoanguka sasa, na ulimwengu wote kuporomoka, hata hivyo sisi tunabatizwa katika Ufalme usioweza kutikisika. Amina. Tunapokea Ufalme. Kwa hiyo, ulimwengu ukiporomoka, tunazaliwa katika Ufalme huu usioweza kuporomoka. Ni Neno

la Milele la Mungu, nasi tunasimama juu ya hilo. Haliwezi kuporomoka kamwe.

157 Sisi tunasikia mengi sana kuhusu mfumo huu mpya unaenda kuleta, mfumo wa kidini, mnajua, unaenda kuleta amani duniani, wakati Katoliki na Waprotestanti wote watakapoungana pamoja. Baadhi yao wanaamini katika uponyaji wa Kiungu, wengine hawaamini, na wengine wanaamini *hili*, na wengine wanaamini *lile*. Na inakubidi kuacha mzozo wenu mkubwa mmekuwa mkizozania wakati wote, imani yako ya kiinjilisti, kuingia katika Baraza la Ulimwenguni. Basi kila dhehebu itabidi liingie hapo ndani. Kwa hiyo, kama dhehebu limelaaniwa, na kuwa mshiriki wake, kunafanya nini? Kunakutupa moja kwa moja nyuma. Kama Rumi ndiyo mama wa dhehebu, na yeye ndiye mnyama na alama ya mnyama, basi walifanya sanamu kwake, baraza, makanisa yote pamoja yanafanya sanamu kwa mnyama huyo, kwa hiyo moja kwa moja kurudi kwenye alama ya mnyama tena! Mfumo wa ulimwengu, umadhehebu, umeinua mfumo kuleta alama ya mnyama.

158 Na wewe unaiona sawa na vile ninavyoiona mimi, kwamba sasa hivi inaenda kulazimishwa, kwamba, wote ambao hawako ndani ya hiyo iliyowekwa katika utaratibu tayari, mashine kubwa iliyowekwa pale; mitambo ipo pale ikimngojea Shetani aingie ndani yake, akiwa na nguvu tendaji. Mnaona? Na, wakati ikifanya, hakuna mtu awezaye kuhubiri Injili, hakuna mtu, pasipo kuwa mshiriki wa mfumo huu. Hiyo hapo alama ya mnyama. Pia kumbukeni, kwenye wakati huo, Bibi-arusi ameenda, kwa hiyo unaona jinsi ilivyo karibu. Vema, kwa hiyo unaona mahali tulipo.

159 Unaweza kuona nini: huu mporomoko mkubwa, mambo haya wanayoendelea kuyahusu. “Loo, amkeni, enyi watakatifu wa Bwana, kwa nini msinzie huku mwisho unakaribia?” Kwa nini mnafanya hivyo? Wakati mwingine mnaondolea mbali siku yenu ya neema kwa kutenda dhambi. Kamwe msifanye hivyo. Naam, bwana.

160 Sasa, mfumo huu hautaleta amani ya ulimwengu. Kama huo utaleta amani ya ulimwengu, ni nini kilichomfanyikia Mfalme wa Amani ambaye alikuwa ni Neno? Ni upinga Kristo katika mafundisho yake. Unapinga yale hasa ambayo Mungu alisimamia, yale Yeye aliyotuambia. “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio,” wanaamini huo ni upuuzi. Matendo 2:38 ni kitu kingine, kwao, hawajui chochote kukihusu. Neno lote, na kadhalika, hawajui chochote kuhusu Hilo, na wanalikana Hilo. Inatimiza hasa kile nabii alichosema katika Timotheo wa Pili, mlango wa 3, “Watakuwa wakaidi, wenye kujisifu, wenye mfano wa utauwa, na wangekana Nguvu zake, katika siku za mwisho.”

161 Mfumo huo wa kimadhehebu ndio alama ya mnyama. Mmejua. Kama hukuwahi kunisikia nikisema hilo hapo kabla, hiyo ndiyo sababu nimeitikisa kwa nguvu sana. Kwa sababu sasa ninafikiri wakati karibu umekwisha, kwa hiyo ninaweza tu kuiacha ije na kusema Kweli kuhusu hilo. Huyo hapo. Huko ndiko kutiwa alama ya mnyama, hasa. Rumi ilikuwa ndiyo mnyama, na yeye alikuwa ni dhehebu, shirika la kwanza.

162 Nasi tulitoka ndani yake, sisi watu Wapentekoste, ili kutokuwa washirika wake; na kugeuka na kurudi moja kwa moja, "kama mbwa kwa matapiko yake, na nguruwe kwenye kugaagaa kwake," moja kwa moja kurudi ndani. Si ajabu mfumo wetu wa Kipentekoste umekwisha, na ndivyo na wa Methodisti, wa Baptisti, Baraza la Makanisa Ulimwenguni, na yote! Wanamezwa katika Baraza la Makanisa, wakifanya alama ama—ama sanamu ya mnyama, kumpa uweza wake. "Naye alikuwa na kichwa chenye jeraha la mauti, na kisha akaishi," Rumi ya kipagani hadi Rumi ya kipapa. Loo, jamani, jinsi Waprotestanti wamekuwa vipofu! Na wewe upo hapa, sasa unaketi moja kwa moja katikati yake. Na hakuna kitu uwezacho kufanya sasa. Mfumo umeundwa tayari. Wataichukua na wasijue wameichukua. Watakuwa tu humo ndani, hayo tu. Hawawezi kutoka katika huo. Imefanyika tayari.

163 Si geni kwa watu, hata hivyo. Limeshahubiriwa. Kumbukeni, Mungu alitoa ushuhuda wake, akalithibitisha kwa Neno Lake. Mambo ambayo Yeye alisema angefanya, Yeye aliyafanya hakika. Kwa hiyo, haina udhuru. Naam.

164 Ni mitambo bandia. Imeleta vitu hasa kile Yesu alichofanya, "Nyinyi kwa mapokeo yenu mmelitangua Neno la Mungu." Kwa kulikataa hilo Neno la kweli, wamerudi moja kwa moja ndani ya kitu hicho tena, mafundisho yao na kitu kile kile kama walivyokuwa hapo mwanzo, na, huko kumpinga Kristo, kulifundisha Neno kwa waaminio katika wakati huu na kuwaambia ku—kukataa na kukana.

165 Wakati Mungu alipolifanya Neno Lake mwili miongoni mwa watu Wake, katika wakati wa Yesu Kristo, kwenye Krismasi ya kwanza, makundi ya Kifarisayo yalifanya nini pamoja na madhehebu hayo yote? Kasema, "Hata msiende kwenye moja ya mikutano hiyo. Ukienda, utatengwa wakati utakapofanya hivyo."

166 Hivi hamwoni jinsi mambo yalivyojirudia moja kwa moja tena? "Ni nani Mtu huyu? Alikuja kutoka shule gani? Ana kadi gani ya ushirika? Ana kundi gani? Ametoka wapi Mtu huyu?" Kama, Yeye amekuja leo kama alivyofanya wakati ule. "Hatutakubali Mtu huyu atutawale. Hatutakubali mtu yeyote atuambie la kufanya. Sisi ni Umoja. Sisi ni Utatu. Sisi ni Presbiteri. Sisi ni *hili*. Haitulazimu kuvumiliana na Hilo!"

167 Ninajua haiwalazimu, lakini ama mtalichukua Neno au mwangamie! Hayo tu. Hiyo si njia nyingine ila Hilo, bali Hilo ndilo linalotushikilia pamoja. Ufalme wa Mungu si ufalme wa huu, sio, Ufalme wa Mungu sio mfumo wa ulimwengu huu. Yesu alisema hivyo. Yesu alisema, "Ufalme wangu si wa ulimwengu huu. Kama ungalikuwa, wajumbe Wangu wangepiga vita." Yeye ni Neno.

168 Sisi ni kama Ibrahimu. Ibrahimu alipokea Neno. Na chochote kilichokuwa kinyume na Neno, alikiita kana kwamba hakikuwepo. Na mtoto yeyote wa Mungu aliyezaliwa kweli hupokea Neno la Mungu, na, sijali kile mtu yeyote asemacho, ni mfumo gani unaonena dhidi ya hilo Neno, Neno ni kweli, kwa vyovyote.

169 Mungu anawajibika kukutana na wewe juu ya msingi wa hizo ahadi. Nje ya ahadi hizo, Yeye hawezi kukutana na wewe, kwa sababu tayari umejikatilia mbali kutoka Kwake. Hiyo ndiyo sababu ulimwengu wetu unaporomoka. Katika kufunga, huenda tukasema hili.

170 Chochote kilicho kinyume na Hilo, ni kana kwamba hakikuwepo. Mfumo kama huo ulioundwa na mwanadamu, kamwe hatuangalii huo. La, bwana. Tukibatizwa basi katika Ufalme huu, tumeketi sasa katika mahali pa Mbinguni katika Kristo Yesu, loo, jamani, pamoja na Mfalme wetu aliyepakwa mafuta pamoja nasi; tukila Ufalme Wake, Neno lililoahidiwa ambalo limetiwa upako na kuthibitishwa moja kwa moja miongoni mwetu. Amina. Whiu! Hiyo hapo, ahadi ya Ufalme Wake ikifanywa moja kwa moja mbele zetu, hakuna kitu kinachoweza kukugeuza kutoka Kwake. La, bwana.

171 Ibrahimu, ingawa mke wake amezeeka, na yeye akizidi kuzeeka wakati wote, haikumsumbua hata kidogo. Hakusitasita kwenye ahadi ya Mungu, kwa kutokuamini. Haijalishi ni kiasi gani unasema, "Haiwezekani. Hawezi kupita na hiyo," alidumu na Hilo, kwa vyovyote. Kwa sababu gani? Mfalme alikuwa pamoja naye, akimwonyesha maono na kumwonyesha yale yatakayokuja kutimia, na ikatokea kama tu Yeye alivyosema, na yeye alijua huyo alikuwa ni Mungu.

172 Basi wakati Mungu anapotoa ahadi nawe unaiona, na Yeye anaisema na inatukia, na kusema na inatukia, na kusema, inatukia, nayo haishindwi, ni Mungu kwa ajili ya siku hiyo. Loo, tukila ahadi hizi za Kimbinguni za Neno Lake lililoahidiwa kwa ajili ya wakati huu, loo, tukijua, pamoja na uhakika kamili wa imani, kwamba kunakuja mbingu mpya na nchi mpya. Amina. "Mbingu mpya na nchi mpya, kwa kuwa mbingu hii ya kwanza na nchi ya kwanza zitapita." Bali katika mbingu hii mpya na nchi mpya, Paulo alisema hapa katika Kitabu cha Waebrania, ninii ya ishirini-. . .14:25, alisema, "Kwa kuwa tunapokea Ufalme usioweza kutetemeshwa." Tuliingiaje ndani yake? Si kwa mfumo

wa kidini; bali, Ufalme wa Mungu uko ndani yenu. Ule Ufalme! Mfalme na Neno Lake ni kitu kile kile, na Hilo liko ndani yenu, likithibitisha saa ambayo sasa tunaishi. Ahadi ambayo Mungu alifanya kwa ajili ya wakati huu, sisi hapa, tunaishi na Mfalme, tukiketi katika mahali pa Mbinguni, tukimwona Yeye akifanya mambo haya.

173 Basi tunawezaje kugeuka kutoka kwa hilo Neno, kuendea mfumo fulani? Huo unafanya nini? Unalikataa Neno. Inakubidi kupokea kuikataa Kweli, kabla hujaweza kuchukua makosa. Hiyo ni kweli kabisa. Je! mnaamini hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

174 Saa tunayoishi, Ee Mungu, ulimwengu unaporomoka! Kule kunaning'inia kwenye mabanda, mabomu, kule kunaning'inia kitu cha kufanya hivyo hasa.

175 Kanisa liko tayari. Ametiwa muhuri ndani, tayari kuja. Kutakuwa na umwagikaji mkubwa wa Roho, naam, bwana, kulinyakua Kanisa hilo na kumpeleka Huyo angani. Hakika. Kwa sababu, unaona, Kanisa, Neno, Bibi-arusi . . . Na, Kristo, huduma Yake iko ndani ya Bibi-arusi Wake, ambaye ni Mwili Wake, Mwili wa kimbinguni, ama ninamaanisha kusema, Mwi— Mwili Wake wa kimbinguni hapa kwenye mwili wa kiroho duniani, Roho Wake yumo humo ndani akiishi Maisha Yake moja kwa moja, hadi Yeye na Kanisa wanakuwa mmoja katika ndoa. Unaona, wanakuwa mmoja. Yeye anawachukua, maskini wachache tu katika siku za mwisho.

176 Ndipo basi mabikira hao wote waliolala, kote katika wakati, wote walifufuka, mnaona. Sasa, hiyo ni katika zamu ya saba, wakati wa saba wa kanisa, wa mwisho, wakati wa mwisho, Laodikia, kwenye mwisho, wakati kundi dogo tu la hao lilipoingia. Lakini, inaleta ufufuo wote wa wale wote waliokufa katika nyakati zao, wakiishi kwa Neno hilo ambalo lilikusudiwa na Mungu na kuhubiriwa kutokea katika siku hiyo, kama tulivyopitia nyakati hizo za kanisa na kuona hasa lile Neno ambalo lingekutana nao katika wakati huo; jinsi ambavyo Luther aliinuka, jinsi tunavyoona, katika wakati wa Luther, alitokea mnyama kama uso wa mwanadamu juu yake, na kuenenda, ambaye alikuwa ni "mrekebishaji," kumaanisha *mwanadamu*. Pia, wakati, nyakati zote, kila mmoja ulitimiza tu hasa kwa matakwa ya Neno la Mungu.

177 Na vivyo hivyo wakati huu utakutana moja kwa moja na ishara na maajabu na jambo ambalo Mungu aliahidi kufanya katika siku hizi za mwisho. Na Kanisa Lenyewe litakuwa tayari na litaenda katika Unyakuo pamoja na Yesu, kwa sababu, "Tunapokea Ufalme usioweza kutetemeshwa. Hauwezi kutikiswa. Mbingu na nchi zitapita, bali Ufalme huu kamwe hautapita." Amina. Nina furaha kuwa, usiku wa leo, amina, usiku wa leo, katika Ufalme huo. Hivi nyinyi hamna furaha

kuwa ndani ya Huo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Loo, jamani, kuwa katika Ufalme, Huo!

178 Wazia tu, ungeweza kujiahidi nini mwenyewe leo hii? Katika miaka mingine kumi hadi kumi na mitano, kama ulimwengu utasimama, kama ukisimama muda huo, kila mwanaume katika Shreveport, kila mwanamke, itakubidi kubeba bunduki, barabarani, pamoja nawe, mfukoni mwako, kujikinga. Majambazi! Utakomeshaje hilo? Jaribu hiyo. Vema, ninii yote . . .

179 Nilikuwa huko New York, wiki ile nyingine. Na kushuka kupitia pale, maili nyingi, hakukuwa na kitu ila hawa tineja majambazi wakiwa na vipuli katika masikio yao, na nywele timtimu, wamevaa legotadi, nao wasichana wakiwa na bikini ndogondogo, walivyoiita, wameivaa namna hiyo, nje mtaani. Nao umma lazima uwapishe njiani. Loo, kuna shida gani katika nchi hii? Ni kwa sababu ni i—ishara ya kuoza kimaadili, taifa lililomkataa Mungu. Hayo tu.

180 Unawezaje kujenga juu ya vifusi vya maangamizi fulani namna hiyo? Unaendaje kufanya hilo, wakati majambazi wanatembea barabarani na kupiga risasi Rais mwenyewe moja kwa moja kutoka kwenye gari lake?

181 Halafu usiku mwingine, mtu wa kilabuni, tayari kufanya ghasia na kila kitu, alitembea moja kwa moja kuingia na kuruka mbele za kikosi cha polisi cha Texas kukiwa na zaidi ya mia moja na kitu wamesimama pale, akaingia moja kwa moja; na kila mtu akimtazama, akavuta bunduki yake na kumpiga mtu risasi katika mauaji ya kikatili, na kutoka akitembea. Atajitetea kuwa ni "mwendawazimu," na kuachiliwa huru.

182 Moja kwa moja katika jiji letu, mtu aliingia moja kwa moja kwenye gareji, hivi majuzi, katika njama ndogo, na kuchukua m—m—mtu aliyekuwa m—mwuza magari. Hakumpenda, ndipo akavuta tu bunduki na kumpiga risasi, mara nne au tano. Naye akasema alikuwa ni mwendawazimu; wakamwacha aende. Kama ni "wendawazimu" anaotetewa mtu huyo, basi pia Oswald alikuwa na fursa, angepaswa kuwa na fursa ya kujitetea kuwa ni mwendawazimu.

183 Ni kitu gani, hata hivyo? Unaona mahali ilipo, kitu hicho chote ni lundo kubwa la uozo! Kitu chote kina hatia, na ulimwengu wote unasimama ukiwa na hatia, nalo kanisa linasimama likiwa na hatia mbele za Mungu. Amina. Si ajabu tunaporomoka!

Na tuombe.

184 Bwana Mungu, sisi hawa hapa. Saa imewadia, Baba. Huenda ikawa imechelewa kuliko tunavyowazia. Labda uozo umeingia sana, na parare amekuwa akila, na madumadu, mpaka Uhai wote umetoweka. Ninakuomba Wewe, Bwana, kuturehemu. Jalia, Bwana, kama kuna mwanaume au mwanamke, mvulana

au msichana, katika Uwepo sasa, wasiokujua Wewe, kwamba watakukubali Wewe hivi sasa, Baba. Huenda ndilo jina la mwisho ambalo litapata kuingia kwenye Kitabu, kutoka Shreveport.

185 Na huku tukiwa tumeinamisha vichwa vyetu. Je! mtu huyo yupo hapa angeweza kuinua mkono wako, useme, "Ndugu Branham, nimeshawishika kabisa kwamba yale uliyosema ni kweli. Ulimwengu unaporomoka, nasi tunapokea Ufalme usioweza kuporomoka. Tena, kwangu mimi, sina hakika kama niko ndani ya Ufalme huo, au la."

186 Usiegemee juu ya kama umekuwa na namna fulani ya kuchochewa kwa msisimko. Usiegemee juu ya kama ulinena kwa lugha. Ninaamini katika mambo hayo. Hakika, ninaamini katika kunena kwa lugha. Lakini nimesikia mashetani wakinena kwa lugha na kutoa fasiri yake, kuandika katika lugha zisizojulikana, wachawi, unaona. Huwezi kutegemea hilo.

187 Lakini ikiwa Uzima wa Yesu Kristo umo ndani yako, Huo utajiishi Wenyewe, ukiamini kila Neno la Mungu. Kwa sababu, Yeye hawezi kujikana Mwenyewe, Yeye ni Neno.

188 Sasa, kama Yeye ni Neno, na Yeye yuko ndani yako, halafu basi unasema, "Vema, Ndugu Branham, nakwambia, siwezi kabisa kuchukua Hilo. Siamini Hili, mambo haya ni kwa ajili ya siku hii," na hapa Hilo limeahidiwa kwa ajili ya siku hii, loo, ndugu yangu, umedanyanyika. Roho fulani amekuja juu yako na kukudanganya.

189 Mama, ikiwa wewe, au mwanaume, au yeyote uliye, ikiwa mambo hayo ambayo ni halisi kabisa, halisi katika Neno, ambayo Yesu Kristo alikufa kwa ajili yake; sio tu kuwa na kanisa au kuwa na kundi la msisimko, bali kuwa na kundi ambalo lina Roho Wake, wakiishi ndani Yake; Bibi-arusi Wake, Neno Lake liko humo ndani, kila Neno ni kweli. Na wewe unajua Hilo halitendi kazi kupitia wewe namna hiyo, unajua kuna mambo, katika Biblia, ambayo wewe huwezi tu kuamini kuwa ni hivyo; na unataka kukumbukwa katika maombi? Sasa huku kila jicho limefumbwa, kila kichwa kuinamishwa, sijui, ikiwa kwenye wakati huu uliochelewa ambapo . . .

190 Huenda karibu umepita wakati wa kuhisi, unaona, kwa sababu kutakuja wakati kama huo ambapo Roho wa Mungu ataondolewa duniani, hatakuwepo tena. Kanisa litabaki kwa muda, hiyo ni kweli, likihubiri, maana halina budi kuwahubiria waliopotea Milele, kama tu ambavyo kila huduma ilifanya, kushuka chini kupitia wakati. Sehemu ya mwisho ya kila huduma ilihubiria waliopotea Milele. Basi kutakuwa na huduma sasa ambayo itawahubiria waliopotea Milele baada ya wao kukataa kupokea Hilo.

191 Lakini ikiwa bado kunabakia kuwa na mwali moyoni mwako, kwamba ungetaka kuwa na Kristo ndani yako,

na ulimwengu wote umekufa, naomba uinue mkono wako, useme, “Nikumbuke katika maombi, Ndugu Branham.” Bwana awabariki. Naam, naam, mikono kumi au kumi na mitano. Huenda kuna mwingine kabla hatujaomba? Sasa tunaandaa kufunga, katika yapata dakika mbili au tatu. Mungu akubariki, msichana.

192 Hebu wazia tu hilo, waza, wazia hilo, vipi kama ingekuwa imechelewa kupita kiasi? Vipi kama wewe ndiye mtu wa mwisho ambaye Yeye atawahi kubisha mlangoni?

193 Unaporomoka, tunajua hilo. Huwezi kubaki hapa, hilo ni jambo moja hakika. Huwezi kubaki hapa. Unaenda. Shikilia tu hilo, unaenda. Na kama wewe ni . . .

194 Usisisimkwe tu. Usiseme, “Mimi ni mshiriki wa kanisa.” Wewe kuwa na hakika na Hilo. Ikiwa Kristo haishi wewe, ndani yako, mpaka wewe ni . . . nia yako yote, moyo, nafsi, mwili.

195 Wewe, unasema, “Vema, nafikiri . . . ” Huna wazo lolote linalokuja, ndugu. Hebu na nia iliyokuwa ndani ya Kristo iwe ndani yako! “Nafikiri siku hazipaswi kuwa . . . Nafikiri *hili* halipaswi kuwa. Nafikiri Neno halimaanishi *hili*.” Hatuna wazo lolote linalokuja.

196 Kama nia ya Kristo iko ndani yetu, basi tutalitambua hilo Neno kuwa ni Kweli, na Hilo linaishi moja kwa moja kupitia sisi. Huwezi kuzuia, Hilo ni Kristo!

197 Chukua uhai kutoka kwenye shina la tikitimaji na kuutia ndani ya shina la boga, utazaa tikitimaji. Huwezi kuuzuia kufanya hivyo, maana ndio uhai ulio ndani yake.

198 Na kama—na kama ukisema, “Vema, siamini Hilo, Ne—Neno hapa,” basi huyo si Roho wa Kristo. Unaona, yupo roho mwingine ndani yako.

199 Kuna mwingine kabla hatujaomba? Mungu akubariki. Mungu akubariki, na wewe, wewe. Naam, hilo ni jema. Sasa, mtu mwingine, dakika moja tu sasa. Mungu akubariki, ewe kijana. Wewe, msichana. Wewe, dada. Mungu akubariki, na wewe. Vema, yupo mwingine? Mungu akubariki, huko nyuma.

200 Usiogope sasa. Usione haya sasa. Kesho usiku huenda ikawa umechelewa kupita kiasi. Unaona? Huenda ikawa ni usiku wa leo moyo huo utakapoacha kudunda. Huenda ikawa usiku wa leo ambapo ulikataa Hilo, mara yako ya mwisho.

201 Ni wangapi humu ndani ambao hawana ubatizo wa Roho Mtakatifu, inueni mikono yenu, unajua kwamba—kwamba hunaye Huyo? Jamani! Hivyo ndivyo unavyoingia. Roho Mtakatifu ni Kristo. Hivyo ndivyo unavyotiwa muhuri katika Ufalme, Waefeso 4:30, “Msimhuzunishe Roho Mtakatifu wa Mungu, ambaye kwa yeye mmetiwa muhuri hadi siku ya ukombozi wenu.” Na kama wewe—na kama wewe una mawazo

ya Biblia hii, kwamba Hii si kweli, basi roho iliyo ndani yako si Kristo, maana Kristo ni Neno.

202 Huo hapo Ufalme usioweza kutikisika, hilo ni Neno. Huo ndio Ufalme usioweza kutikisika. "Mbingu na nchi zitapita, bali Neno Langu halitapita." Ikiwa Neno liko ndani yako! "Mkikaa ndani Yangu, na Neno Langu ndani yenu; ombeni mtakalo, mtatendewa. Kazi nizifanyazo," Yohana Mtakatifu 12, 14, "kazi nizifanyazo, mtazifanya pia; hata nyingi kuliko hizi, kwa sababu ninaenda kwa Baba. Bado kitambo kidogo, na ulimwengu hautaniona tena; bali ninyi mtaniona, kwa kuwa nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hadi mwisho wa ulimwengu."

203 Angalia kile kazi Zake zilichokuwa, uone kama kimeturudia katika siku za mwisho. Je! wamekataa Hilo? Kote ulimwenguni! Na ulimwengu unaporomoka tena, Krismasi hii, kama ilivyokuwa Krismasi ile.

204 Baba yetu wa Mbinguni, kulikuwa na mikono mingi iliyoinuliwa hapa usiku wa leo, labda thelathini ama arobaini, katika kundi hili dogo la watu, iliinuliwa usiku wa leo, kwamba walijua hawakuwa hasa mahali wanapaswa kuwa. Walijua kwamba Wewe hukukaa ndani yao, katika Kipimo. Wengine, labda kitu fulani katika Biblia, wanasema, "Ninanii tu... ni—ni—ninakubali Hilo kwa sababu ni—ninafikiria tu kwamba labda ninapaswa kufanya hivyo."

205 Lakini, Bwana, Wewe uliahidi kwamba Wewe ungekuwa ni Neno, na Wewe ni Neno. "Ndipo mimi nitakuja kwako, na kujijulisha Mwenyewe kwako." Tunaona kwamba mifumo Yako, mfumo Wako, haubadiliki kamwe.

206 Wakati Wewe ulipokuja katika Agano la Kale, Wewe ulisema, "Neno liliwajia manabii." Na Hilo lilipokuja, walitabiri na Hilo likatimia, kwa kuwa Hilo lilikuwa ni Mungu.

207 Sasa tunatambua kwamba wakati Wewe ulipotutuma kwenda, na kutuagiza kuenda ulimwenguni kote na kufanya wanafunzi, na Wewe ulisema, "Wakati Yeye Roho Mtakatifu atakapokuja juu yenu, Yeye atawakumbusha mambo hayo, niliyowafunza." Hiyo ni kusema, tena! "Na atawaonyesheni mambo yanayopaswa kuja." Bado! "Mungu, katika zama za kale na kwa njia mbalimbali alinena na baba zetu kupitia manabii; katika siku hizi za mwisho kupitia Mwana Wake, Kristo Yesu." Roho Mtakatifu Mwenyewe, akija, Mfunuaji wa Neno lililoandikwa, na Mwonyeshaji wa mambo yajayo! Ilisema, "Neno la Mungu," katika Waebrania 4, "ni kali kuliko upanga ukatao kuwili, Tambuzi la mawazo yaliyoko moyoni."

208 Na mwenye dhambi na mtu wa kanisa, leo hii, anaweza kuketi na kukuona Wewe ukifanya jambo lile lile, na kuita Hilo roho *mwovu*, kama tu walivyofanya katika siku zilizopita.

"Ikiwa wamemwita Bwana wa nyumba 'Beelzebuli,'" nasi tunaona hilo.

209 Bwana, Mungu, ni nini zaidi tuwezacho kufanya sasa? Ipo mioyo yenye njaa hapa iliyoinua mikono yao. Wachukue sasa hivi, Bwana, jaza kila moyo na upendo Wako. Tujalie hayo.

210 Na huku tukiwa tumeinamisha vichwa vyetu. Ikiwa nyinyi mlioinua mikono yenu mngependa kuja karibu na jukwaa hapa, usi—usiliweke kando, unaona. Dakika hii tu inayofuata sasa, simama tu moja kwa moja, upesi sana, na uje hapa, simama tu. Huu huenda ukawa ndio usiku utakaompokea Roho Mtakatifu.

211 Marafiki, tazameni, hii haitakuwa nyakati zote. Hiyo, hiyo inaenda kuisha. Inamalizika sasa hivi, na huenda imemalizika tayari. Lakini mradi tu mnajaribu kutamani kumjia Kristo, basi hakika kuna kitu hapo, bado, kinachowavuta upande huo.

212 Hivi hutakuja sasa na usimame papa hapa kwa ajili ya maombi? Nyinyi mnaotamani kufanya hivyo, mnaweza kutembea moja kwa moja huku karibu na madhabahu, kwa muda mfupi tu, huku tungali tumeinamisha vichwa vyetu. Sasa watu wanakuja moja kwa moja huku juu. Hiyo ni kweli, njoni moja kwa moja karibu na madhabahu. Useme, "Ulimwengu unaporomoka, sitaki ulimwengu wowote ndani yangu. Ninataka Ufalme ndani yangu, usioweza kuporomoka."

213 Yesu alisema, "Hakuna chochote kitakachopotea. Nitakifufua tena katika siku za mwisho. Naam, nitakifufua." Yeye aliahidi, kwa hiyo huwezi kuporomoka. Mungu anaenda kukifufua. Sijali ni kitu gani, Yeye anaenda kukifufua.

214 Hivi ulijua kwamba hakuna kitu kinachoweza kuangamizwa na mwanadamu? Hakuna kitu kinachoweza kuangamizwa. Unasema, "Vipi kuhusu moto, wakati unapoteketeza kitu?" Haukiangamizi. Ni atomu humo ndani zinavunjavunja hizo kemikali, ndipo unapata moto kutoka kwake. Zinarudi moja kwa moja katika hali yake ya asili, jinsi zilivyokuwa hapo mwanzo; asidi, gesi, nuru, na kadhalika, kama zilivyokuwa. Huwezi kuangamiza chochote. Kama—kama ulimwengu ungesimama muda mrefu vya kutosha, huenda kikarudi kuwa kijipande kingine cha karatasi, au mti mwingine, au chochote unachoteketeza. Unaona, huwezi kukiangamiza. Mungu ameiweka hivyo.

215 Loo, huwezi kuangamiza kiumbe cha Mungu, hiyo ni kweli kabisa, kwa hiyo ni kiasi gani Yeye anaweza kufufua kile ambacho Yeye ameahidi!

216 Hivi hutakuja? Je! kutakuwa na wengine zaidi sasa? Lipo kundi dogo hapa, si nusu ya wale walioinua mikono yao. Nilidhani mlimaanisha kweli mlipoinua mikono yenu, hasa juu ya Ujumbe kama huo.

217 Ni wangapi wenu hapa ndani, sasa huku vichwa vyenu vimeinamishwa, wanajua hili, kwamba mmemwona Mungu akitimiza ahadi Yake, papa hapa kwenye jukwaa hili, na kujua siri za moyo? Mmoja, hakuna hata wakati mmoja Yeye aliwahi kusema chochote ila kile kilichotendeka. Mnajua hiyo ni kweli. Katika mikutano, kila mahali, kile hasa ambacho Yesu Kristo alifanya wakati Yeye alipokuwa hapa duniani, Yeye amekifanya tena. Mnajua hilo. Mnajua hilo. Nilikuwa nikiwazia uponyaji Wake.

218 Majuma mawili yaliyopita, kabla sijaenda New York, kulikuwa na mama fulani aliyekuja akiwa na kansa kooni. Roho Mtakatifu akamzungumzia, kwenye mkutano. Hapa alikuwepo, Jumapili, akiwa na kansa kwenye kijipande cha kitambaa, alikuwa ameikohoa ikatoka. Madaktari waliiangalia, na kusema, "Uhai ulitoka ndani ya kansa hiyo, nayo ikawa legevu." Ndipo akaikohoa ikatoka.

219 Mwingine alikuwa na kansa kwenye tezi za kike. Na alikuwa nayo pale pale, kwa picha iliyopanuliwa, pamoja na maelezo ya daktari pamoja nayo. Alikuwa ameipita, siku mbili baadaye.

220 Jamaa mmoja mdogo akiwa amesimama pale, ambaye hakuwa amekuwa na kumbukumbu, tangu—tangu miezi na miezi na miezi. Alikuwa ameanguka na kuumiza upande wa nyuma ya kichwa chake. Hata hakujua kuwa yeye alikuwa ni nani au mahali alipokuwa. Kwa neno tu la maombi, na kuweka mikono juu yake, nikasema, "Jina lako nani?"

Akasema, "Billy Dukes."

Nikasema, "Una umri gani?"

Akasema, "Umri wa miaka tisa." Kasema, "Niko wapi?"

221 Nguvu za Mungu! Laiti mngalikuwa pamoja nami huko Colorado, majuma machache yaliyopita, wakati jambo fulani lilipotukia ambalo lingewatetemesha, kujua kuwa lilikuwa ni kitu gani. Tuko wakati wa mwisho, ewe rafiki.

Kamwe, kamwe usiweke hili kando kwa muda wowote mwingine. Njoo. Iwapo kuna mwingine hapa, njoo huku. Hivi utakuja? Utakuja?

222 Sasa, iwapo huji, unaona, si—siwezi, mimi—mimi—mimi—mimi. . . Yote niwezayo kufanya ni kukwambia tu Kweli, unaona, halafu ni juu yako. Kama vile Nuhu, aliingia ndani, safina ikajifunga nyuma yake, hakuna kilichotendeka kwa muda; lakini ulimwengu uliangamia huko nje, nao ulimwengu uliendelea tu kuishi vile vile. Unaona?

223 Pilato aliendelea moja kwa moja, baada ya yeye kumsulubisha Yesu. Nitahubiri juu ya hilo, katika siku chache usiku, "damu mikononi mwako," Bwana akipenda.

Angalia sasa, je! kuna mwingine, kabla hatujafunga?

224 Sasa ninaenda kuwaomba wanawake na wanaume halisi waliojiweka wakfu, wanaomjua Mungu, washuke chini na kusimama hapa na kuweka mikono juu ya watu hawa. Huu huenda ikawa ndio wakati wa mwisho ambao watawahi kuwa na fursa hii. Baadhi yenu watu mliojiweka wakfu ambao mnamjua Mungu, njoni huku na msimame pamoja na watu hawa. Wanazo kadi za rangi ya waridi juu yao, karibu kila mmoja wao, hiyo inamaanisha kwamba wao ni, wao ni wageni miongoni mwenu. Nafikiri hiyo ni kweli. Njoni, wekeni mikono yenu juu yao. Baadhi ya washiriki wa Maskani ya Uzima, njoni hapa. Baadhi yenu ndugu hapa juu mnataka kuja? Njoni, huu ndio wakati. Hivi hamninii—hivi hampendi hili, enyi watu? Jamani! Wapi juhudi zetu? Wapi kile kitu chetu fulani ambacho hutufanya kusogea? Kuna shida gani?

Sasa ikiwa wasikilizaji watangojea kwa dakika moja tu, kwa maombi haya.

225 Enyi watu mnaosimama hapa, sasa angalieni, msiegemee mhemko fulani, ingawa lina mhemko ndani Yake. Usiegemee juu ya ikiwa utanena kwa lugha, au la. Usiwazie chochote juu yake. Mungu atashughulikia hayo, unaona. Wewe mwombe Yesu Kristo aje ndani ya maisha yako na kujiishi Mwenyewe kupitia wewe. Hutaki tena mawazo yako mwenyewe. Unataka mawazo Yake. "Hebu ile nia iliyokuwa ndani ya Kristo iwe ndani yenu." Loo, hili ni . . .

226 Hili, vema, unaenda tu kusikia mambo haya kwa mara ya mwisho, siku moja. Sasa tazama, ninataka wasikilizaji wote kusimama kwa miguu yenu, hapo nje. Sasa, enyi watu wapendwa mliokuja hapa juu kwa ajili ya ubatizo wa Roho Mtakatifu, kesho ni kutoa Shukrani, hakuna kufanya kazi kesho. Hii ni nafsi yako, ndugu, dada. Hii ni hatima yako ya Milele. Hii, ama ni sasa au sivyo kamwe. Na mradi tu unahisi mvuto huo mdogo! Pia wazia tu Kweli hizi, zipo moja kwa moja mbele zetu. Usiwe mfu juu ya mambo hayo, jamani. Ni halisi. Imethibitishwa, halisi, kamilifu kila wakati. Nalo ni Neno, lililothibitishwa!

227 Ninamwangalia mwanamume aliyesimama papa hapa. Siwezi kulikumbuka jina lake. Ninaamini ni Blair, Kasisi Blair. Nilipokuwa huko Hot Springs, hapa si muda mrefu uliopita, nilitambua huko katika wasikilizaji, mtu yule anayeketi pale, na roho mwovu alikuwa akijaribu kumfikia mtu huyo, kumfanya anitilie shaka. Sasa angalia kilichofanyika. Nilisema, "Huenda ukanihitaji wakati mwingine, unaona." Haikuwa ila majuma machache yaliyopita mpaka mke wake akanipigia simu, mtu huyo alikuwa anakufa. Unaona?

228 Ndipo mtu huyo akakubali, alijua hapo ilikuwa ni ibilisi akijaribu kumfanya kuamini kuwa Hilo lilikuwa ni namna fulani ya udanganyifu au kitu kingine. "Lakini yeye angejuaje

jambo hilo?" akawazia. Kwa hiyo basi yeye. . . Kwa maombi tukautorosha uovu huo kutoka kwake.

229 Halafu basi majuma machache yaliyopita, unaona, Shetani alijua kwamba wakati huo ulikuwa unakuja, ambapo angekuwa amelala pale akiwa na uvimbe ubavuni mwake, ninaamini mke wake alisema, ama kitu fulani, akiwa na homa kali, akiwa na mapayo kichwani mwake; sijui kilikuwa ni kitu gani, akiwa na maambukizo fulani ubavuni mwake, ukafanya ubavu wake kuvimba. Ndipo maskini mke wake akanipigia simu huko Tucson. Nikasema, "Dada, je! una leso?" Ninaamini alikuwa na kitu fulani pale, skafu ndogo au kitu fulani. Nikasema, "Ni—ninaweza kuiona. Chukua hii ukaiweke juu ya Ndugu Blair, katika Jina la Bwana Yesu." Na yeye alikuwa amemwomba mke aje apige simu.

230 Vipi kama Shetani angalifaulu na kumfanya kutoamini, akijua kwamba hiyo ilikuwa hapo? Asingalikuwa amesimama hapa usiku wa leo akiwa na Biblia yake juu ya moyo wake. Unaona?

231 Ni Shetani akijaribu kukufanya kutokuamini Hili. Hiyo ni kweli. Usisikilize hilo. Kumbukeni, "Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele." Unaona, mambo haya yamethibitishwa hivyo.

232 Sasa hebu sisi sote, nyinyi hapa kwenye madhabahu, hebu tuinue tu mikono yenu, na kusema, "Bwana Yesu, nisaidie sasa hivi," kila mmoja akiomba.

233 Baba yetu wa Mbinguni, tumekusanyika hapa, Ee Mungu, ni kati ya mauti na uhai, kwa watu hawa wanaosimama hapa. Jalia Roho Mtakatifu aje ndani ya maisha yao sasa hivi. Jalia Nguvu za Mungu zije, ambazo zimewaleta hapa juu karibu na hii madhabahu, jalia Hizo ziwajie katika ufufuo wa Kristo, na zitawapa ule Uzima mkuu wa Milele ambao wanautafuta. Bwana, makanisa kila mahali yanakufa, maji ya kiroho yanaonekana kuondolewa duniani. Na wakati kukiwepo na fursa kwa ajili ya watu hawa kuja chini ya ile Chemichemi, jalia, Bwana, kwamba nafsi zao zilizo na kiu, usiku wa leo, zilizo na njaa na kiu kwa ajili ya Mungu, zipate kujazwa na Roho Mtakatifu sasa hivi. Tujalie hayo, Bwana. Jalia rehema Zako na neema ziwe juu yao.

234 Sasa ninii tu—endelea tu kukiweka kichwa chako . . . endelea kuomba, endelea tu kuomba. Kila mtu, unaona, endeleeni tu kuomba. Ninawaombeeni. Nitafanya yote niwezayo, ila siwezi kuwapatia Roho Mtakatifu. Mungu hana budi kufanya hilo. Tazama, umba Kristo moja kwa moja mbele zako, niani mwako. Angalia huko nje na uone kama unamwona Kristo mbele zako, unapofumba macho yako. Halafu utembee moja kwa moja kuingia ndani Yake, na useme, "Bwana Yesu, mimi hapa. Wewe na mimi tunaenda kuwa mmoja, tangu sasa na kuendelea.

Nitachukua kila Neno ambalo Wewe umeniambia usiku wa leo." Sasa bakia tu hapo, endelea tu kukaa, ukikaa usiku wa leo, kesho, siku inayofuata, kaa tu mpaka yote yaishe, ukiomba, ukiamini kwamba Mungu atakujaza na ubatizo wa Roho Mtakatifu.

235 Njoo hapa, Don, waongoze katika maombi. Mungu akubariki, Don.

*Ulimwengu Unaporomoka Tena* SWA63-1127
(The World Is Again Falling Apart)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumatano jioni, tarehe 27 Novemba, 1963, katika Maskani ya Life kule Shreveport, Louisiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2019 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

Voice Of God Recordings
P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org